# SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR
# WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE

# HOTUBA YA BAJETI YA WAZIRI WA UTALII NA MAMBO YA KALE

**MHESHIMIWA MUDRIK RAMADHAN SORAGA (MBM),**

**KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA, KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 AKIWASILISHA MBELE YA BARAZA LA WAWAKILISHI**

**MEI, 2025**

## YALIYOMO


YALIYOMO ............................................................................i
VIFUPISHO VYA MANENO ............................................iv
A. UTANGULIZI.....................................................................1
B. MUUNDO NA MAJUKUMU YA WIZARA...................3
MUUNDO WA WIZARA.......................................................3
MAJUKUMU YA WIZARA.................................................4
C. MAPATO YALIYOKUSANYWA NA WIZARA KWA KIPINDI CHA MIEZI TISA (JULAI 2024-MACHI 2025)...........................................................................5
D. MAFANIKIO YA WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE KWA SERIKALI YA AWAMU YA NANE KUANZIA 2020 HADI 2025 ..............................5
SEKTA YA UTALII ..............................................................6
SEKTA YA MAMBO YA KALE ........................................11
E. CHANGAMOTO ZA WIZARA NA HATUA ZA UTATUZI ...................................................................................14
F. FEDHA ILIYOPATIKANA KWA KIPINDI CHA MIEZI TISA (JULAI 2024-MACHI 2025) .........................16
G. PROGRAMU KUU ZA WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE .....................................................17
H. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 ...........................18
I. UTEKELEZAJI WA BAJETI ZA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA WIZARA KWA JULAI 2024-MACHI2025 ......................................................................25
I. PROGRAMU YA MAENDELEO YA MAKUMBUSHO, MAMBO YA KALE NA UHIFADHI WA MJI MKONGWE ..............................................................................25

UTEKELEZAJI HALISI ........................................................26
II. PROGRAMU YA KUSIMAMIA MAENDELEO YA UTALII............................................................................30
UTEKELEZAJI HALISI ........................................................31
III. PROGRAMU YA UTANGAZAJI NA UHAMASISHAJI UTALII ...............................................34
UTEKELEZAJI HALISI ........................................................34
IV. KURATIBU NA KUSIMAMIA MAENDELEO YA UTALII ...................................................................36
UTEKELEZAJI HALISI ........................................................37
UTEKELEZAJI HALISI ........................................................39
V. PROGRAMU YA UENDESHAJI NA MIPANGO KATIKASEKTA YA UTALII NA MAMBO YA KALE......40
UTEKELEZAJI HALISI ........................................................41
UTEKELEZAJI HALISI ........................................................44
UTEKELEZAJI HALISI ........................................................47
J. VIPAUMBELE VYA WIZARA KWA MWAKA 2025/2026. ...................................................................49
K.MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA2025/2026 .................................................50
L. KUWASILISHA BAJETI YA MFUMO WA PROGRAMU(PROGRAM BASED BUDGET - PBB) KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 .............................52
Programu ya Kwanza: Programu ya Maendeleo ya Makumbusho, Mambo ya Kale na Uhifadhi wa Mji Mkongwe ..........................................................53
Programu ya Pili: Programu ya Kusimamia Maendeleo ya Utalii...........................................................54

Programu ya Tatu: Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji Utalii......................................................56
Programu ya Nne: Programu ya Uendelezaji na Uratibu wa Utalii......................................................57
Programu ya Tano: Uendeshaji na Mipango katika Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale .................................60
M. SHUKURANI ......................................................65
N. MAOMBI YA FEDHA KWA AJILI YA KUTEKELEZA PROGRAMU ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 ......................................................69
O. HITIMISHO......................................................71
VIAMBATISHO ......................................................72
Kiambatisho namba 1A......................................................73
Kiambatisho Namba 1B......................................................74
Kiambatisho Namba 1C......................................................77
Kiambatisho Namba 1D......................................................79
Kiambaticho Namba 1E......................................................80
Kiambatisho Namba 1F ......................................................83
Kiambatisho Namba 1G......................................................85
KIAMBATISHO 2 ......................................................86

# VIFUPISHO VYA MANENO

| | |
|---|---|
| CCM | Chama Cha Mapinduzi |
| CHICOP | Chumbe Island Coral Park |
| EU | European Union |
| GSTC | Global Sustainable Tourims Council |
| HAZ | Hotel Association Of Zanzibar |
| IIT | Indian Institutes Of Technology |
| ITB | Internationale Tourismus Borse |
| JICA | Japan Intenational Coorperation Agency |
| LTD | Limited |
| MICE | Meeting Incentive Conference And Exibition |
| MoU | Memorandum Of Understandings |
| NMB | National Microfinance Bank |
| PBB | Program Based Budget |
| PBZ | Peoples Bank Of Zanzibar |
| PDB | Presidential Delivery Beuro |
| SMZ | Serikali Ya Mapinduzi Zanzibar |
| TANAPA | Tanzania National Park |
| TBI | Tony Blair Institute |
| TEHAMA | Teknolojia Ya Habari Na Mawasiliano |
| TSA | Tourism Settellite Account |

| | |
|---|---|
| TTB | Tanzania Tourism Board |
| UNCDF | United Nations Capital Develeopment Fund |
| UNDP | United Nations Development Programme |
| UNECA | United Nations Economic Commission For Africa |
| UNESCO | United Nations Education Sciences |
| UNICEF | United Nations International Children Emergence Fund |
| UNIDO | United Nations Industrial Development Organization |
| USAID | United States Agency For International Development |
| ZADEP | Zanzibar Development Plan |
| ZATI | Zanzibar Association Of Tourism Investors |
| ZATO | Zanzibar Assiciation Of Tour Operators |
| ZATOGA | Zanzibar Tour Guide Association |
| ZBC | Zanzibar Broadcasting Cooperation |
| ZTIS | Zanzibar Tourism Investment Show |

# HOTUBA YA BAJETI YA WAZIRI WA UTALII NA MAMBO YA KALE, MHESHIMIWA MUDRIK RAMADHAN SORAGA (MBM), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA MWAKA WA FEDHA 2025/2026, AKIWASILISHA MBELE YA BARAZA LA WAWAKILISHI

## A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** naomba nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu muumba mbingu na ardhi, kwa kuendelea kuturuzuku neema ya uzima na uhai na kuweza kutukutanisha tena leo hii katika muendelezo wa vikao hivi vya kujadili Makadirio na Matumizi ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Makadirio hayo yanalenga kutekeleza Malengo na Majukumu ya Wizara huku tukizingatia maslahi mapana ya wananchi wa Zanzibar. Tunamuomba Mwenyezi Mungu atuongoze vyema katika kutekeleza jukumu hili pamoja na kutupa Hekima, Busara, Uaminifu na Uadilifu wakati wa kutekeleza majukumu yetu ya kila siku.

2. **Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee, naomba nichukue fursa hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyeketi wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuiongoza vyema nchi yetu huku akihakikisha kwamba analeta Mapinduzi makubwa ya maendeleo na kukuza uchumi wa nchi. Mapinduzi haya ya Maendeleo yamekuwa yakiwagusa wananchi wote wa visiwa hivi vya Unguja na Pemba katika harakati zao za maisha ya

kila siku. Aidha, niendelee kumpongeza kwa kushirikiana nasi katika jitihada za kuitangaza Zanzibar Kimataifa kupitia ziara zake za kushiriki katika Makongamano, Maonesho na Matamasha ya Kitalii yanaoendelea kufanyika katika mataifa mbali mbali, ambayo yanachangia kukuza uchumi wa nchi. Aidha, niendelee kumpongeza kwa kuitekeleza kwa vitendo Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2020 - 2025, ambapo utekelezaji wake umevuka malengo. Tunamuomba Mwenyezi Mungu amjaalie Mheshimiwa Rais wetu afya njema pamoja na kumzidishia Hekima, Maarifa na Uadilifu wakati akiendelea kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

3. **Mheshimiwa Spika,** kwa ruhusa yako, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Othman Masoud Othman, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar pamoja na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, kwa kuchapa kazi kwa kiwango cha hali ya juu na kumsaidia Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyeketi wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi katika kufanikisha utekelezaji wa malengo ya nchi pamoja na kuendelea kuibakisha nchi yetu katika hali ya Umoja, Upendo na Mshikamano huku tukijivunia Amani na Utulivu uliotawala ambao unatuletea maendeleo ya kasi, kuelekea katika Uchaguzi Mkuu ujao wa Oktoba 2025. Niwaombe wananchi wote waendelee kuitunza tunu hii ya umoja na amani iliyopo katika nchi yetu wakati tukikabiliwa na uchaguzi Mkuu wa Urais, Wabunge, Wawakilishi na Madiwani. Ninamuomba Mwenyezi Mungu atujaalie uchaguzi wa Salama na Amani.

4. **Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua nafasi hii adhimu, kukupongeza wewe Spika wa Baraza la Wawakilishi pamoja na wasaidizi wako wote akiwemo Naibu Spika, Mwenyekiti wa Baraza, Katibu wa Baraza, Wenyeviti wa Kamati, Wajumbe wa Baraza, Maofisa na Wafanyakazi wote wa Baraza la Wawakilishi kwa jitihada za hali ya juu wanazozitumia katika kufanikisha majukumu na malengo ya Baraza hili.

## B. MUUNDO NA MAJUKUMU YA WIZARA

5. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale imeundwa kwa lengo la kusimamia Sekta Kuu mbili ambazo ni Utalii na Mambo ya Kale. Vile vile, Wizara hii imepewa majukumu ambayo huyatumia katika kupanga malengo ya Idara na Taasisi zetu.

### MUUNDO WA WIZARA

6. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale inasimamia Taasisi na Idara zifuatazo : -

i. Idara ya Uendeshaji na Utumishi

ii. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti

iii. Idara ya Utalii

iv. Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale

v. Kamisheni ya Utalii Zanzibar

vi. Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe

vii. Ofisi Kuu Pemba

## MAJUKUMU YA WIZARA

7. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale pamoja na mambo mengine pia inatekeleza majukumu yafuatayo: -

i. Kuitangaza Zanzibar kiutalii ndani na nje ya nchi.

ii. Kukuza pato la Taifa kupitia Sekta ya Utalii.

iii. Kuwashawishi wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuanzisha miradi ya utalii na urithi wa kihistoria itakayotoa tija kwa wananchi.

iv. Kusimamia na kuendeleza hifadhi ya Mji Mkongwe ambayo ni eneo la urithi wa kimataifa la UNESCO.

v. Kusimamia na kuendeleza makumbusho ya kihistoria na mambo ya kale ikiwa ni pamoja na kuratibu masuala ya urejeshaji wa malikale kutoka nje ya nchi.

vi. Kuyalinda, kuyahifadhi na kuyatangaza maeneo ya urithi wa kihistoria yaliyopo nchini.

vii. Kuvitunza vitu na mabaki ya kihistoria yaliyopo nchini ili kuweka kumbukumbu kwa faida ya kizazi cha sasa na kizazi kijacho.

## C. MAPATO YALIYOKUSANYWA NA WIZARA KWA KIPINDI CHA MIEZI TISA (JULAI 2024-MACHI 2025)

8. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale katika mwaka wa fedha 2024/2025 ilipangiwa kukusanya **Shilingi 1,239,894,000**/= na hadi kufikia Machi 2025 imefanikiwa kukusanya **Shilingi 1,194,286,408**/= sawa na **asilimia 96.3%.** Ni matarajio yetu kuvuka lengo la makusanyo haya kwa asilimia 100 pindi mwaka wa fedha 2024/2025 utakapokamilika. Fedha zote hizi zimeingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Aidha, kupitia Kamisheni ya Utalii ambayo mapato yake hutumia kwa ajili ya shughuli za utangazaji utalii pamoja na uendeshaji wa ofisi imepanga kukusanya **Shilingi 12,825,262,611**/= na hadi kufikia Machi 2025 imefanikiwa kukusanya **Shilingi 6,610,724,909**/= sawa na **asilimia 51. (Tafadhali angalia kiambatisho namba 1A)**.

## D. MAFANIKIO YA WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE KWA SERIKALI YA AWAMU YA NANE KUANZIA 2020 HADI 2025

9. **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Awamu ya Nane inayoongozwa na Jemedari, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi imeshika madaraka ya nchi hii mnamo Novemba mwaka 2020. Kutoka kipindi hicho hadi sasa mwaka 2025 kupitia Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale, Wizara imetekeleza mambo mengi. Miongoni mwa mafanikio hayo ni kama ifuatavyo: -

## SEKTA YA UTALII

### i. Kuongezeka kwa Matamasha Yanayotangaza Vivutio vya Utalii Zanzibar

Matamasha ya kutangaza utalii nchini yameongezeka kutoka wastani wa matamasha matatu kwa mwaka hadi kufikia 10 mwaka 2024. Kwa mfano: Tamasha la Uwekezaji na Utalii, Fahari ya Zanzibar, Tamasha la Vyakula vinavyopandwa bila ya kutumia mbolea au viuatilifu vya kemikali yaani "Organic". Tamasha la Kizimkazi, Zanzibar Holiday Market Festival, Trace Music Awards, Halal Tourism Festival, Tamasha la Vyakula vya Asili (Makunduchi) na Tamasha la Utalii na Utamaduni (Pemba Tourisport Bonanza and Culture). Kuongezeka kwa matamasha haya nchini kunasaidia kwa kiasi kikubwa kuitangaza nchi yetu kitaifa, kikanda na kimataifa pamoja na kukuza idadi ya watalii wanaoingia nchini.

### ii. Kuongezeka Uwekezaji katika Miradi ya Utalii

Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inaendelea kuweka mazingira rafiki ya uwekezaji nchini kwa kutunga Sera, Sheria pamoja na kuweka miongozo mbali mbali inayorahisisha hatua za uwekezaji nchini. Kutokana na juhudi hizi uwekezaji katika sekta ya utalii umeongezeka kutoka miradi ya kitalii 995 iliyosajiliwa katika mwaka 2020 hadi kufikia miradi 1,695 sawa na ongezeko la **asilimia 70.4%** katika mwaka 2024. Aidha, miradi hii inamilikiwa na wazalendo, wageni au ubia baina ya wazalendo na wageni. Miradi husika ni mahoteli, mikahawa, miradi ya mawakala wa utalii "tour operators",

kumbi za mikutano, maduka ya zawadi (Souvenir Shops) na michezo ya baharini.

iii. **Kukua kwa Utalii wa Michezo**

Kutokana na jitihada zinazofanywa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar za kuongeza matukio ya kuwavutia watalii nchini, zimepelekea kukuwa kwa utalii wa michezo. Miongoni mwa michezo maarufu inayochezwa kwa sasa ni mashindano ya  kurusha vishada (kite surfing) Mbio za Masafa Marefu (Marathon), Michezo ya Mbio za Masafa Marefu zikichanganywa na Mbio za Baiskeli na Kuogelea (Triathlon), Mpira wa Ufukweni (Beach Soccer) na Mpira wa wavu wa Ufukweni (Beach Volleyball). Kufanyika kwa michezo hii nchini kumesaidia kuitangaza Zanzibar kimataifa na kupelekea kuongezeka kwa idadi ya wageni wanaoingia nchini.

iv. **Kuongezeka kwa Idadi ya Watalii Wanaoingia Nchini**

Kutokana na jitihada zinazofanywa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar za kuitangaza Zanzibar kiutalii ndani na nje ya nchi, kumekuwa na ongezeko kubwa la idadi ya watalii wanaoingia nchini kwa mwaka, kutoka watalii 260,644 mwaka 2020 hadi kufikia watalii 737,775 mwaka 2024. Ongezeko hili ni sawa na **asilimia 65%.**

v. **Kukua kwa Taasisi Binafsi Zinazosaidiana na Serikali Kusimamia Sekta ya Utalii.**

Katika kuimarisha sekta ya utalii nchini, Serikali kwa kushirikiana na Taaasisi Binafsi imeimarisha na kusimamia

Jumuiya ya Wawekezaji wa Sekta ya Utalii ambazo ni (ZATI), Jumuiya ya Upangaji wa Misafara ya Watalii (ZATO) na Jumuiya ya Waongozaji Watalii (ZATOGA). Aidha, katika kipindi hiki cha uongozi wa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar, kumezinduliwa Jumuiya inayosimamia maslahi ya wenye hoteli za kitalii Zanzibar (HAZ). Uwepo wa Jumuiya hizi ni muhimu sana katika kuendeleza sekta ya utalii kwa vile huwa ndio Daraja muhimu baina ya wawekezaji na Serikali.

vi. **Kuwa na Mfumo wa Upimaji wa Pato la Taifa katika Sekta Utalii (Tourism Satellite Account)**

Kwa mara ya kwanza Wizara kwa kushirikiana na Kamisheni ya Umoja wa Mataifa inayoshughulikia Uchumi Barani Afrika (UNECA) imeandaa Mfumo wa Upimaji wa Mchango wa Utalii kwenye Pato la Taifa (Tourism Satellite Account). Kukamilika kwa mfumo huu kunawezesha kujulikana mchango halisi wa utalii katika Pato la Taifa. Tayari ripoti hiyo imeshatolewa na imeshaanza kutumika. Kutokuwepo kwa mfumo huu kulipelekea kutolewa taarifa zilizokuwa hazikuakisi mchango halisi wa sekta ya utalii kwa Pato la Taifa. Kuwepo kwa mfumo huu kutatuwezesha kutambua mchango halisi wa sekta ya utalii katika Pato la Taifa zaidi ya kipimo cha sasa cha kutumia mfumo wa kawaida wa GDP ambao kwa sasa ni **asilimia 29.2%.**

vii. **Kutengenezwa kwa Filamu za Kutangaza Vivutio vya Utalii vya Zanzibar za "The Royal Tour na Presidential Tour"**

Wizara iliratibu zoezi la uchukuaji na utengenezaji wa Filamu ya "The Royal Tour" kwa upande wa Zanzibar, ambapo filamu hii, iliwashirikisha kikamilifu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Aidha, Wizara ilimpokea msanii maarufu kutoka nchini China, Jin Dong aliyeambatana na wasanii wengine, waliofika nchini kwa lengo la kutayarisha filamu iliyomshirikisha Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Filamu hii inajulikana kwa jina la "Presidential Tour." Hivi karibuni tulipata ugeni wa wasanii maarufu kutoka India wakiongozwa na Shakti Mohan na kutengeneza filamu ya Tantalizing Tanzania. Pamoja na filamu nyengine kadhaa ambazo zimetengenezwa kuitangaza Zanzibar, filamu hizi zimesaidia kwa kiasi kikubwa kutangaza vivutio vya nchi na kupelekea kuongezeka maradufu idadi ya watalii wanaoingia nchini.

viii. **Zanzibar Kushinda na Kutunukiwa Heshima Mbali Mbali za Utalii Duniani**

Zanzibar imekuwa ikirishiriki katika matukio ya kimataifa ambayo hujishughulisha na utoaji wa tunzo mbali mbali za utalii kwa nchi au kisiwa kinachofanya vizuri zaidi ya visiwa vyengine. Kutoka mwaka 2020 hadi kufikia mwaka

2025 Zanzibar imefanikiwa kupata tunzo sita za utalii ambazo ni “Africa Tourism Board of the Year” mwaka 2022, “Africa’s Leading Beach Destination” mwaka 2022, “4th Top Destination in Africa” mwaka 2024, “9th World Top Honeymoon Destination” mwaka 2024, “Best Romatic Destination” mwaka 2024 na “2nd Best Island Holidays” mwaka 2024. Kupatikana kwa tunzo hizi kumepelekea kuitangaza zaidi Zanzibar kimataifa na kuongezeka kwa idadi ya watalii wanaokuja kutembelea nchini.

ix. **Kuongezeka kwa Safari za Moja kwa Moja za Ndege kutoka Mataifa Mbali Mbali duniani**

Zanzibar imekuwa ikipokea safari za moja kwa moja za ndege kutoka mataifa mbali mbali duniani. Ujio huu wa ndege za moja kwa moja unatokana na kufunguliwa kwa Jengo jipya lenye huduma bora zaidi za Kimataifa za Abiria la Terminal III katika Uwanja wa Ndege wa kimataifa wa Abeid Amaan Karume. Aidha, kuongezeka kwa safari za moja kwa moja ndani ya kipindi hiki cha Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kumetokana na juhudi kubwa zinazochukuliwa na Serikali yetu ya Awamu ya Nane ya kuongeza ushiriki wa Zanzibar katika maonesho, matamasha na makongamano ya Kikanda na Kimataifa ya kuitangaza Zanzibar pamoja na vivutio vya utalii vilivyokuwemo nchini. Miongoni mwa mashirika ya ndege yaliyoanza kuja Zanzibar katika Awamu hii kwa safari za moja kwa moja ni pamoja na Shirika la Ndege la Royal Dutch Airlines (KLM), Edelweiss Air, Air France, TUI na Hi Fly. Mashirika haya yameweza kuiunganisha zaidi Zanzibar

na nchi nyingi. Hali hii imefanya uingiaji zaidi wa wageni kutoka nchi mbali mbali kama vile Ufaransa na Uholanzi na kwengineko katika bara la Ulaya uwe rahisi zaidi. Hivi sasa Zanzibar ni fikio la wageni wengi ambao hapo awali walishindwa kufika kwa sababu hawakuwa wakifurahia safari za kuunganisha.

**x. Kuongezeka kwa Idadi ya Hoteli za Daraja la Juu**

Katika kipindi cha miaka mitano (2020-2025) kumekuwa na ongezeko la idadi ya hoteli za daraja la juu (nyota 5 na 4) kutoka hoteli 54 mwaka 2020 hadi kufikia hoteli 79 mwaka 2025 ambayo sawa na ongezeko la asilimia 32.

## SEKTA YA MAMBO YA KALE

**i. Kuimarika kwa Uwekezaji katika Maeneo ya Kihistoria na Mambo ya Kale**

Kwa miaka mingi maeneo haya ya kihistoria na mambo ya kale yalikuwa katika hali mbaya kwa sababu ya kukosa wawekezaji. Chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt Hussein Ali Mwinyi na hususan katika kuleta kwake mpango madhubuti wa mageuzi katika sekta ya Mambo ya Kale, kwa sasa, maeneo mengi ya kihistoria na Mambo ya Kale yamepatiwa wawekezaji kwa lengo la kuyaimarisha ili yaweze kuendelezwa na kutunzwa historia ya maeneo hayo kwa faida ya kizazi cha sasa na kizazi kijacho, pamoja na kuyafanya maeneo hayo kuwa ni vivutio vya utalii. Miongoni mwa maeneo ya kihistoria na Mambo ya Kale

yaliyopatiwa wawekezaji ni pamoja na eneo la kihistoria la Fukuchani, eneo la kihistoria la Ngome Kongwe, eneo la kihistoria la Chuini, eneo la kihistoria la Maruhubi, eneo la kihistoria la Mtoni, iliyokuwa Mahakama Kuu ya Zanzibar, Mahamamu ya Kijichi, Forodhani na Hamamni, bustani za Mnazi Mmoja na Africa House na majengo ya Saravan Karai.

ii. **Kufanyika kwa tafiti za Akiolojia Unguja na Pemba ili kujua upana wa historia iliyopo katika maeneo ya visiwa vyetu**

Wizara imekuwa ikishirikiana na taasisi za elimu ya juu za kitaifa na kimataifa katika jitihada za kufanya tafiti kubwa za akiolojia, kwa lengo la kufahamu kwa kina historia ya sehemu husika. Tafiti hizi huwashirikisha wataalamu wa ndani na nje ya nchi. Maeneo ambayo yamefanyiwa utafiti ni pamoja na eneo la kihistoria la Chwaka, eneo la kihistoria la Dunga, eneo la kihistoria la Ngome Kongwe, eneo la kihistoria la Mkokotoni pamoja na maeneo ya Kizimbani, Machui, Kombeni, Maungani, Jumbi, Kama, Bububu na Mwakaje. Tafiti hizi zimegundua mambo mengi ya kihistoria ambapo awali mambo hayo yalikuwa hayatambuliki.

iii. **Kuyafanyia matengenezo makubwa maeneo ya kihistoria**

Wizara imekuwa ikendelea kutekeleza programu ya kuyaimarisha na kuyaendeleza maeneo ya kihistoria yaliyopo nchini. Katika kipindi hiki cha miaka mitano ya Serikali ya awamu ya nane, Wizara imefanikiwa kufanya matengenezo

makubwa kwa maeneo ya kihistoria ya Makumbusho ya Mnazi Mmoja, eneo la kihistoria la Mangapwani, Pango la Watoro na pango la Kijiji, eneo la kihistoria la Chwaka Tumbe na eneo la kihistoria la Ras Mkumbuu. Kuendelea kuyafanyia matengenezo maeneo ya kihistoria ni hatua moja wapo ya kutunza na kuhifadhi historia iliyopo nchini kwa faida ya kizazi cha sasa na kijacho.

**iv. Kuimarika kwa utekelezaji wa miradi ya uhifadhi na uendelezaji wa Mji Mkongwe**

Serikali ya awamu ya nane imekuwa ikuchukua juhudi za makusudi za kuimarisha eneo la Mji Mkongwe kwa kutekeleza miradi ambayo huleta mvuto katika eneo hilo, miradi inayotekelezwa katika eneo hilo husimamiwa na kutolewa ushauri wa kitaalamu na Wizara, kwa lengo la kuifanya miradi hiyo iendane sambamba na dhana ya uhifadhi na uendelezaji wa Mji Mkongwe ili uendelee kubakia kuwa urithi wa Kimataifa. Miradi ambayo imetekelezwa katika kipindi hiki cha awamu ya nane na kusimamiwa na Wizara ni pamoja na ukarabati wa Soko kuu la Darajani, Mradi wa Darajani Souk, Ukarabati wa Jengo la Old Dispensary na Ukarabati wa Makaburi ya Wafalme wa Oman yaliyopo "Palace Museum". Wizara kupitia Mamlaka ya Mji Mkongwe inaendelea na kazi ya ukarabati wa jengo la Beit el Ajaib, Jumba la Wananchi (People's Palace), Ikulu ya Kibweni kwa kushirikiana na Serikali ya Oman, UNESCO na majengo mengine yaliyopo ndani ya Mji Mkongwe kwa kushirikiana na Serikali ya Morocco.

v. **Kushirikisha wananchi katika kuyatunza, kuyahifadhi na kuyatumia maeneo ya u Mambo ya kale.**

Maeneo mengi ya kihistoria kwa sasa yamezungukwa na jamii ambazo zipo karibu na maeneo hayo. Kutokana na umuhimu wa maeneo hayo kwa faida ya Serikali na nchi kwa ujumla, Wizara imeimarisha jitahada za kuwashirikisha wananchi na jamii kwa ujumla kwa kuwapatia elimu ya uhifadhi na utunzaji wa vitu na maeneo ya kihistoria na Mambo ya Kale. Elimu hiyo imekuwa ikitolewa kupitia vyombo vya habari na mikutano ya wazi.

## E. CHANGAMOTO ZA WIZARA NA HATUA ZA UTATUZI

10. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale licha ya kufanikiwa katika malengo na majukumu yake iliyojipangia pia inakabailiwa na changamoto mbalimbali kama ifuatavyo:-

| Nam | Changamoto | Hatua zilizochukuliwa |
|---|---|---|
| 1. | Utalii wa misimu unaosababisha kupanda na kushuka kwa idadi ya watalii na vyanzo vya mapato | Wizara imefanya juhudi ya kuongeza wigo wa fursa mbali mbali za kuvutia watalii bila kujali misimu kama vile utalii wa michezo, utalii halali, utalii wa mikutano, utalii wa vyakula pamoja na utalii wa urithi na utamaduni |
| 2. | Uhaba wa wataalamu katika sekta ya Utalii na Mambo ya Kale | Wizara inaendelea kuwasomesha wataalamu wa sekta ya Utalii na Mambo ya Kale katika ngazi mbali mbali kwa lengo la kuwaongezea utaalamu na ujuzi kazini. |

| | | |
|---|---|---|
| 3. | Ushiriki hafifu wa vikundi vya jamii katika programu mbali mbali za sekta ya Utalii | Wizara inaendelea kushirikiana na wadau mbali mbali wa maendeleo katika kubuni na kutekeleza miradi mahsusi inayolenga wanajamii na wajasiriamali wadogo wadogo ili waweze kunufaika katika kauli mbiu yetu ya Utalii kwa Wote |
| 4. | Uelewa mdogo wa wanajamii katika hatua za uwekezaji wa miradi ya kimkakati hususan katika sekta ya Utalii | Wizara inaendelea kutoa elimu shirikishi kwa wanajamii kuhusiana na umuhimu na faida ya uwekezaji kwa ajili ya maendeleo endelevu yanayowashirikisha kwa ukamilifu |
| 5. | Uhaba wa Wawekezaji wa Sekta binafsi katika masuala ya Mambo ya Kale | Wizara inaendelea kushirikiana na Wawekezaji wa sekta hii kupitia mpango wake wa mageuzi unaohusisha na uanzishwaji wa Sheria inayounda Mamlaka ya Usimamizi wa Makumbusho na Mambo ya Kale. |
| 6. | Uvujaji wa mapato katika vyanzo vya vivutio vya Utalii na Mambo ya Kale | Wizara kwa kushirikiana na wadau mbali mbali wa taasisi za fedha imeanzisha na kuboresha mifumo ya kidijitali ya malipo inayoziba mianya ya upotevu wa mapato. |
| 7. | Upatikanaji wa fedha za Miradi ya Maendeleo katika sekta ya Utalii na Mambo ya Kale | Wizara inashirikiana na Tume ya Mipango katika kufuatilia upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo inayotekelezwa kupitia sekta ya utalii na Mambo ya Kale, kupatikana kwa wakati kwa fedha hizo kutachangia kukamilika kwa miradi katika muda uliopangwa. |
| 8. | Ukiukwaji wa masharti ya vibali kwa wamiliki wa nyumba za Mji Mkongwe ambao huzifanyia matengenezo nyumba hizo kinyume na utaratibu. | Wizara imeanzisha mfumo maalum wa utoaji vibali na leseni kwa lengo la kuyafanyia matengenezo majengo yote yaliyopo Mji Mkongwe. |

| | | |
|---|---|---|
| 9. | Uhaba wa vitendea kazi kwa Kikosi cha Polisi Utalii na Diplomasia | Wizara imeendelea kushirikiana na wadau wa maendeleo kwa kuwapatia vitendea kazi kwa Polisi Utalii ili waweze kutekeleza majukumu yao. Kwa mfano, hivi karibuni Taasisi ya ZATI iliikabidhi Wizara Pikipiki za kufanyia doria. Halikadhalika, Ubalozi wa Uingereza nchini Tanzania uliikabidhi Wizara Pikipiki na Magari maalumu ya kufanyia doria za fukwe (All Terrain Vehicles) kwa ajili ya kuimarisha Usalama wa wageni na mali zao |
| 10. | Uvamizi katika maeneo ya kihistoria yaliyopo nchini | Wizara inaendelea kuchukua hatua za makusudi za kuyapima na kuyahifadhi maeneo ya kihistoria na kuyapatia hati miliki |

## F. FEDHA ILIYOPATIKANA KWA KIPINDI CHA MIEZI TISA (JULAI 2024-MACHI 2025)

11. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale iliidhinishiwa fedha za matumizi na Baraza la Wawakilishi **Shilingi 47,032,992,000**/= kwa ajili ya kutekeleza programu kuu tatu na Miradi ya Maendeleo ya Wizara. Kati ya hizo **Shilingi 3,418,800,000/=** kwa kazi za kawaida, **Shilingi 4,588,370,000**/= kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 39,025,022,000**/= kwa kazi za Maendeleo. Kati ya hizo **Shilingi 24,000,000,000**/= zinatoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na **Shilingi 15,025,822,000**/= zinatoka Serikali ya Ufalme wa Oman kwa ajili ya matengenezo ya jengo la Beit el Ajaib. Aidha, Kamisheni ya Utalii iliidhinishiwa makusanyo ya matumizi ya **Shilingi, 12,825,262,611**/=

kwa ajili ya kutekeleza programu kuu mbili, kati ya hizo **Shilingi 2,455,878,711**/= Kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 5,369,383900**/= kwa matumizi mengineyo na **Shilingi 5,000,000,000**/= ni fedha zitakazoingizwa Mfuko Mkuu wa Hazina.

12. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2025, Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale ilipokea jumla ya **Shilingi 5,352,284,026**/= sawa na asilimia 11. Kati ya fedha hizo **Shilingi 1,108,018,891**/= zilipatikana kwa ajili ya kazi za kawaida sawa na **asilimia 32%. Shilingi 3,391,796,433**/= zilipatikana kwa ajili ya mishahara sawa na asilimia 74, na **Shilingi 852,468,702**/= zilipatikana kwa ajili ya utekelezaji wa miradi inayofadhiliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ambayo ni sawa na **asilimia 3.5,** na **Shilingi 6,730,515,103**/= ni fedha kutoka Serikali ya Ufalme wa Oman ambayo ni sawa na asilimia 45. Aidha, Kamisheni ya Utalii ilifanikiwa kupata **Shilingi 1,720,892,686**/= kwa ajili ya mishahara, sawa na **asilimia 70** na **Shilingi 2,371,659,908**/= kwa ajili ya matumizi mengineyo ni sawa na **asilimia 49 (Tafadhali angalia kiambatisho namba 1B).**

## G. PROGRAMU KUU ZA WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE

13. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale inatekeleza Malengo na Majukumu kwa kufuata Mfumo Maalumu wa Bajeti (Program Based Budget, PBB), ambapo Wizara inasimamia programu kuu tano na programu ndogo tatu.

**Programu Kuu za Wizara ni : -**

i. Programu ya Maendeleo ya Makumbusho, Mambo ya Kale na Uhifadhi wa Mji Mkongwe.

ii. Programu ya Kusimamia Maendeleo ya Utalii.

iii. Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji Utalii.

iv. Programu ya Uendelezaji na Uratibu wa Utalii.

v. Programu ya Utawala na Uendeshaji katika Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale.

**Programu Ndogo za Wizara ni: -**

i. Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara.

ii. Utawala na Uendeshaji katika Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale.

iii. Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba.

## H. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWAMWAKA WA FEDHA 2024/2025

**14. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara ilipanga kutekeleza 'Programu ya Kuimarisha na Kuendeleza Maeneo ya Kihistoria' kwa kuyafanyia matengenezo maeneo yafuatayo: -

i. Kuimarisha eneo la kihistoria la Ngome Kongwe – Unguja

ii. Kuimarisha eneo la kihistoria la Maruhubi – Unguja

iii. Kuimarisha Mahamamu ya Kidichi, Kizimbani, Forodhani na Hamamni – Unguja

iv. Kuimarisha eneo la kihistoria la Fufuni – Pemba

v. Kuimarisha eneo la kihistoria la Kichokochwe – Pemba na

vi. Ukarabati wa Majengo Hatarishi ndani ya eneo la Mji Mkongwe

15. **Mheshimiwa Spika,** naomba nichukue nafasi hii kukuarifu kwamba katika jitihada za kutafuta wawekezaji katika maeneo ya Kihistoria na Mambo ya Kale, Wizara imefanikiwa kuipata Kampuni ya "Infinity Developments" ambayo imeingia nayo ubia maeneo ya kihistoria, kwa lengo la kuyaimarisha. Kampuni hiyo tayari imekabidhiwa eneo la kihistoria Ngome Kongwe, Maruhubi, pamoja na Mahamamu ya Kidichi, Hamamni na Forodhani. Pia, mwekezaji huyo amekabidhiwa jengo lilikokuwa Mahakama Kuu ya Vuga. Aidha, eneo la Kihistoria la Fukuchani limepata mwekezaji ambae ni YHM Worldwide Limited.

16. **Mheshimiwa Spika,** kupatikana kwa wawekezaji hawa kumepelekea fedha za Serikali zilizokuwa zitumike katika maeneo hayo ya kihistoria zielekekezwe katika kuwahudumia wananchi kupitia miradi mengine inayotekelezwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

17. **Mheshimiwa Spika,** mara baada ya kupatikana kwa wawekezaji hawa, Wizara imepanga na kukamilisha miradi

mengine ya maeneo ya kihistoria pamoja na kuendelea kutekeleza miradi ifuatayo ambayo ni Ras Mkumbuu na Mangapwani, ambayo utekelezaji wake ulikuwa haujakamailika: -

**Eneo la Kihistoria la Ras Mkumbuu – Pemba**

Mradi wa Kuimarisha Eneo la Kihistoria la Ras Mkumbuu Pemba unatekelezwa na Kampuni ya **Yassin & Sons LTD.** Mradi huu umegharimu **Shilingi 2,407,316,675**/= na hadi kufikia Machi 2025 mjenzi amelipwa **Shilingi 987,871,572.5**/= sawa na **asilimia 41** ya malipo. Utekelezaji wa mradi huu umefikia **asilimia 65** ambapo kazi zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa majengo mapya ya maduka, ofisi, vyoo na mkahawa, kufikisha umeme katika eneo la mradi, uondoshaji wa fusi katika majengo ya kale ya kihistoria pamoja na ukarabati wa majengo ya kale yaliyopo katika eneo hilo. Kazi kubwa inayoendelea kufanyika kwa sasa ni ujenzi wa uzio ili kuzuia mmomonyoko wa majengo unaosababishwa na kuongezeka kwa kina cha maji ya bahari.

**Eneo la Kihistoria la Mangapwani – Unguja**

Mradi wa kuimarisha eneo la Kihistoria la Mangapwani Unguja unatekelezwa na **Al Hilal Company LTD.** Mradi huu umegharimu **Shilingi 2,238,544,230**/= na hadi kufikia Machi 2025 mjenzi amelipwa **Shilingi 1,182,059,623**/= sawa na **asilimia 53** ya malipo na utekelezaji wa mradi huu umefikia **asilimia 90.** Mradi huu unahusisha ukarabati wa maeneo makuu matatu ya kihistoria ambayo ni Kisima cha

Chini kwa Chini, Mabaki ya Mahandaki ya Vita Vikuu vya Pili vya Dunia pamoja na Chemba au Handaki la Kuhifadhia Watumwa. Hadi sasa kazi zilizofanyika katika maeneo haya ni pamoja na ujenzi wa majengo mapya ya maduka, ofisi na mkahawa. Ukarabati wa ngazi za kushukia katika Kisima cha Chini kwa Chini, Ukarabati wa Mahandaki ya Vita Vikuu vya Pili vya Dunia, Ukarabati wa Handaki lililotumika Kuhifadhia Watumwa pamoja na ujenzi wa ukuta kwa ajili ya kuyalinda na kuyahifadhi maeneo ya kihistoria yaliyopo katika eneo hilo.

**Mradi wa Ukarabati wa Nyumba Hatarishi za Mji Mkongwe**

**18.** **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe ilifanya utafiti mdogo wa majengo yaliyopo ndani ya eneo la Mji Mkongwe na kugundua majengo zaidi ya 160 yapo katika hali mbaya na kati ya hayo majengo 36 yapo katika hali mbaya zaidi. Uwepo wa majengo yaliyo katika hali mbaya zaidi ndio yanayopelekea kuanguka kwa baadhi ya majengo na kuleta athari kwa wakaazi wa maeneo hayo pamoja na wageni wanaotembelea kivutio hiki cha urithi wa kimataifa.

**19.** **Mheshimiwa Spika,** katika jitihada za kutatua changamoto za majengo hatarishi yaliyopo ndani ya eneo la Mji Mkongwe, Wizara imewasilisha mradi huu katika mwaka wa fedha 2024/2025 wa ukarabati wa majengo 10 na kutengewa bajeti ya **Shilingi 9,000,000,000**/= na hadi kufikia Machi 2025 mradi huu bado haujaingiziwa fedha za malipo kwa wakandarasi, licha ya utekelezaji wa mradi

huu kwa baadhi ya majengo ukiendelea. Wizara imeanza kuyafanyia matengenezo makubwa majengo manne na utekelezaji wake ni kama ufuatao: -

**Jengo namba 2312 (Jengo la Culture) -Vuga**

20. **Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Ukarabati wa Jengo Namba 2312 lililopo Vuga unatekelezwa na Kampuni ya **K'S Builders Ltd.** Mradi huu unaogharimu **Shilingi 480,470,075.60**/=. Mradi huu umeanza kutekelezwa Novemba 2024 na unatarajiwa kukamilika Mei 2025. Utekelezaji wa mradi huu umefikia **asilimia 89** ambapo kazi zilizofanyika ni pamoja na kurekebisha paa, dari, vyoo, kuweka plasta, kupaka rangi pamoja na kuweka miundombinu mipya ya umeme na maji. Kazi zinazoendelea kwa sasa ni ufungaji wa milango na madirisha pamoja na uwekaji wa sakafu mpya.

**Jengo namba 1196/97 -Malindi**

21. **Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Ukarabati wa Jengo Namba 1196/97 lililopo Malindi unatekelezwa na Kampuni ya **Yassin & Sons Company Ltd.** Mradi huu unagharimu **Shilingi 545,822,200**/=, na utekelezaji wa mradi huu umeanza Disemba 2024 na unatarajiwa kukamilika Juni 2025. Ujenzi umefikia **asilimia 30** ya kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa mujibu wa Mkataba. Kazi zilizofanyika ni pamoja na kulizuiya jengo nje na ndani kwa mirunda ili lisiweze kuanguka, kuzitoa boriti za zamani na kuziweka mpya pamoja na kugonga kuta, kutoa plasta kongwe na kuweka plasta mpya kwa kutumia udongo wa chokaa. Kwa

sasa Mkandarasi anaendelea na kazi za urekebishaji wa paa kwa kutoa mabati ya zamani ili aweke mabati mapya, kuweka sawa miundombinu ya maji na umeme pamoja na urekebishaji wa milango, madirisha na ngazi na hatimae kulipaka jengo lote rangi mpya.

**Jengo namba 1065 –Malindi Funguni**

**22.** **Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Ukarabati wa Jengo namba 1065 lililopo Malindi Funguni unatekelezwa na Kampuni ya **Kin Investment Company Ltd.** Mradi huu unagharimu **Shilingi 742,862,222.5**/=, na utekelezaji wa mradi huu umeanza Novemba 2024 na unatarajiwa kukamilika Mei 2025. Mjenzi tayari ameanza kazi za ukarabati na utekelezaji wake umefikia **asilimia 56.** Kazi zinazofanyika ni kama za jengo namba 1196/97 la Malindi**.**

**Jengo namba F06A – Forodhani**

**23.** **Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Ukarabati wa Jengo namba F06A lililopo Forodhani unatekelezwa na Kampuni ya **Faster Company Limited.** Mradi huu unagharimu **Shilingi 713,680,512.50**/=, utekelezaji wa mradi huu umeanza Januari 2025 na unatarajiwa kukamilika Julai 2025. Tayari mjenzi ameanza kazi na utekelezaji wake umefiki**a asilimia 20.** Kazi zinazotarajiwa kufanyika ni kama za majengo mengine tuliyoyainisha hapo juu.

**Mradi wa Ukarabati wa Beit el Ajaib**

**24.** **Mheshimiwa Spika,** mnamo tarehe 25 Disemba, 2020 sehemu ya jengo mashuhuri la Beit el Ajaib lililoporomoka

na kuathiri jengo hilo. Wastani wa **asilimia 20** ya jengo hili upande wa kaskazini-magharibi lilianguka. Maeneo yaliyoathirika ni sehemu ya kuta za jengo kuanzia ghorofa ya tatu ililosababisha kuanguka kwa varanda (Balcony) ya kaskazini na ya magharibi pamoja na mnara ambao ulioanguka.

25. **Mheshimiwa Spika,** mara baada ya kuanguka kwa jengo hili maarufu, Taasisi na Jumuiya mbali mbali za Kimataifa zilifika nchini kwa lengo la kulikagua upya ili hatua za matengenezo zifanyike kwa mujibu wa uhifadhi wa kimataifa. Baada ya kukamilika ukaguzi wa kina, Serikali ya Ufalme wa Oman ilikubali kulifanyia matengenezo makubwa yanayogharimu Dola za Kimarekani **Milioni 21** na iliingia Mkataba na Kampuni ya "Nandhra Engineering Construction Ltd", wa miaka mitatu kumalianzia Agosti 2023 na unatarajiwa kukamilika Agosti 2026. Hadi Machi 2025, mjenzi ameshalipwa **Shilingi 6,730,515,103**/= sawa na **asilimia 45.** Utekelezaji wa Mradi huu umefikia **asilimia 35,** ambapo mjenzi amefanya kazi za uimarishaji wa msingi, kutengeneza nguzo, kujenga sehemu ya ghorofa ya chini ya ukuta uliyoanguka, kuimarisha kuta na kazi ndogondogo za mbao.

26. **Mheshimiwa Spika,** Wizara itaendelea kuzifanyia ukarabati nyumba hatarishi zilizopo ndani ya eneo la Mji Mkongwe kwa lengo la kuhakikisha kwamba mji huu unaendelea kubaki katika hali ya usalama kwa faida ya wakaazi na wageni. Vile vile, Wizara inaendelea na kazi ya kuyaimarisha maeneo ya kihistoria yaliyopo nchini kwa faida

ya kizazi cha sasa na kijacho. Aidha, kazi za uimarishaji wa maeneo ya kihistoria kunapelekea kuongezeka kwa idadi ya vivutio vya utalii vilivyopo nchini, ambavyo vinachochea ongezeko la mapato ya nchi pamoja na ongezeko la siku za ukaazi kwa wageni wanaoingia nchini.

## I. UTEKELEZAJI WA BAJETI ZA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA WIZARA KWA JULAI 2024-MACHI 2025

**27.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara ilipanga kutekeleza programu kuu tano kama ifuatavyo: -

i. Programu ya Maendeleo ya Makumbusho, Mambo ya Kale na Uhifadhi wa Mji Mkongwe.

ii. Programu ya Kusimamia Maendeleo ya Utalii.

iii. Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji Utalii.

iv. Programu ya Uendelezaji na Uratibu wa Utalii.

v. Programu ya Utawala na Uendeshaji katika Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale.

## I. PROGRAMU YA MAENDELEO YA MAKUMBUSHO, MAMBO YA KALE NA UHIFADHI WA MJI MKONGWE.

**28.** **Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la programu hii ni kuhakikisha uhifadhi na matumizi endelevu ya eneo la urithi la Mji Mkongwe na maeneo ya kihistoria yaliyohifadhiwa,

kuimarishwa na kuendelezwa kwa faida ya kizazi cha sasa na cha baadae. Matokeo ya muda mrefu ni kuyahifadhi, kuyalinda, kuyatangaza na kuyaendeleza maeneo ya kihistoria yaliyopo nchini pamoja na Uhifadhi wa Mji Mkongwe ili kubakia kuwa ni urithi wa kitaifa, kikanda na kimataifa.

29. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ya Uendelezaji wa Makumbusho, Mambo ya Kale na Uhifadhi wa Mji Mkongwe inatekelezwa na Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale na Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe.

30. **Mheshimiwa Spika,** huduma zinazotolewa na programu hii ni Uhifadhi na Uendelezaji wa Makumbusho, Maeneo ya Kihistoria, Mambo ya Kale pamoja na Mji Mkongwe.

## UTEKELEZAJI HALISI

31. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale imefuatilia upatikanaji wa Hati miliki na kufanikiwa kuzipata hati miliki tano za kwa upande Pemba katika maeneo ya Msuka Mjini, Pango la Kijiji, eneo la kihistoria la Mkamandume, Ngome Kongwe na Bustani ya Chake Chake. Pia, Idara imetengeneza mabango sita ya maelezo katika maeneo ya Mkamandume na Chwaka Tumbe. Upatikanaji wa Hati Miliki kwa maeneo ya kihistotria kunasaidia kuyalinda na kuyahifadhi dhidi ya uvamizi wa watu na mifugo unaoufanywa katika maeneo hayo.

32. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua za kujitangaza na kuyatangaza maeneo ya kihistoria Kitaifa, Kikanda na Kimataifa. Idara imefanikiwa kuandaa na kurusha hewani vipindi 37, ambavyo kati ya hivyo vipindi 26 vilirushwa ZBC Redio, vipindi vitano vilirushwa Safari Channel TV, vipindi vitano kupitia Alfatah TV na kipindi kimoja kupitia Zanzibar Cable TV. Pia, Idara imeshiriki katika Maonesho ya Kilimo yaliyofanyika Chamanangwe na Tamasha la Mswahili la kisiwani Pemba. Kwa upande wa Unguja, Idara ilishiriki kwenye Maonesho ya Nane Nane yaliyofanyika Kizimbani, Tamasha la Kizimkazi na Maonesho ya Mapinduzi yaliyofanyika Kisakasaka.

33. **Mheshimiwa Spika,** Idara imepokea jumla ya wageni 37,036 walioetembelea katika maeneo mbali mbali ya kihistoria ambapo kati ya hao 23,418 waliotoka nje ya Tanzania, 2,393 walikuwa ni Watanzania, wageni maalum wa kiserikali ni 45 na wanafunzi kutoka skuli mbali mbali walikuwa 11,180.

34. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua za kuimarisha utendaji kazi pamoja na kukuza utoaji bora wa huduma kwa jamii, Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale imegharamia masomo kwa wafanyakazi wake tisa. Kati ya hao wafanyakazi watatu waliotoka Pemba ambao wawili walisomea "Foundation in Business Administration" na mfanyakazi mmoja alisomea Stashahada ya "Tourism and Heritage Management" katika Taasisi ya Utalii ya Maruhubi. Aidha, Wafanyakazi sita waliotoka Unguja, watatu wamepatiwa mafunzo ya Shahada ya kwanza ya Rasilimali Watu, Shahada ya TEHAMA na

Shahada ya "Record Management". Wafanyakazi watatu wengine, wamepatiwa mafunzo ya Uhasibu, Utunzaji wa Kumbukumbu na "E- Office", wafanyakazi wawili katika masuala ya Makumbusho na Mambo ya Kale.

35. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale, imeendelea kuyatunza na kuyalinda makumbusho kwa faida ya vizazi vya sasa na vijavyo pamoja na wageni wanaotembelea makumbusho hazi. Idara imewapatia chakula, maji na dawa kwa ajili ya kinga za maradhi ndege na kobe waliopo katika Makumbusho ya Mnazi Mmoja pamoja na Kisiwa cha Changuu. Idara lipia huduma za maji na umeme pamoja na kulipia stahiki za likizo na muda wa ziada.

36. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe, imeendelea na kazi ya kurejesha haiba ya maeneo mbali mbali ya Mji Mkongwe kwa kuweka sawa njia za watembea kwa miguu, kuweka vigae (pavements) katika njia na kurejesha haiba ya bustani zilizomo ndani ya Mji Mkongwe kwa kupanda miti ya maua na kuweka taa katika miti yote inayozunguka Uwanja wa Mnazi Mmoja. Sambamba na mambo haya, Mamlaka imeweka pegi kwenye mipaka ya Mji Mkongwe, imezibua na kufunika mitaro, imerekebisha taa na kukata majani kwenye Uwanja wa Mnazi Mmoja.

37. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua za kutoa elimu na ufahamu kwa wananchi juu ya umuhimu wa Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe, Mamlaka imezitembelea skuli sita

za Mji Mkongwe ambazo ni Mkunazini, Kajificheni, Kiponda, Forodhani, Hamamni na Mluka bint Alwy Islamic School na kutoa elimu kwa Walimu na Wanafunzi juu ya umuhimu na faida za Uhifadhi wa Mji mkongwe na athari zitakazopatikana iwapo mji huu ukiondolewa katika Urithi wa Kimataifa wa UNESCO.

38. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka imegharamia mafunzo ya muda mfupi kwa wafanyakazi wanne, ambapo wafanyakazi wawili wamepatiwa mafunzo kuhusu Kodi na Ukaguzi wa Ndani na Uhasibu yaliyofanyika Dar es Salaam na wawili wamepatiwa mafunzo ya Matumizi ya Kisasa ya Zege (Advanced Concrete Technology) yaliyofanyika Chuo cha IIT Madras Zanzibar. Aidha, Mamlaka imewapatia mafunzo ya Usimamizi wa Majanga kwa wafanyakazi wawili nchini Benin. Na imelipa stahiki za likizo kwa wafanyakazi saba na stahiki za malipo baada ya saa za kazi kwa wafanyakazi wanane.

39. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua za kuendelea kuulinda kuuhifadhi na kurithisha elimu kwa vizazi vijavyo, Mamlaka kwa kushirikiana na wadau wa Mji Mkongwe imeendelea kuadhimisha Siku ya Mji Mkongwe kwa mwaka 2024. Maadhimisho haya ambayo hufanyika kila ifikapo tarehe 2 Disemba ya kila mwaka yalihudhuriwa na Viongozi mbali mbali wa Taasisi za Serikali, Asasi za Kiraia, Watu Mashuhuri pamoja na Wananchi waliozunguka eneo la Mji Mkongwe. Mgeni Rasmi katika Maadhimisho hayo alikuwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Dkt. Hussein Ali Mwinyi.

40. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/2025 programu hii ilipangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 42,625,818,712**/= na hadi kufikia Machi 2025 imefanikiwa kupata **Shilingi 9,661,826,787**/= sawa na **asilimia 23, Shilingi 1,025,200,000**/= ziliidhinishwa kwa ajili ya matumizi mengineyo, na hadi kufika Machi 2025 **Shilingi 219,798,135**/= zilipatikana sawa na **asilimia 21.** Vile vile **Shilingi 2,574,396,472**/= ziliidhinishwa kwa ajili ya mishahara na hadi kufikia Machi 2025 imefanikiwa kupata **Shilingi 1,859,044,846**/= sawa na **asilimia 72** ya makadirio. Program hii ilipangiwa **Shilingi 39,025,822,000**/=, kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ambapo kati ya hizo **shilingi 24,000,000,000**/= ni fedha kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na hadi kufikia Machi 2025 imepata **Shilingi 852,468,702**/= sawa na **asilimia 3.5,** na Shilingi **15,025,822,000**/= ni fedha kutoka Serikali ya Ufalme wa Oman na hadi kufikia Machi 2025 imefanikiwa kupata **Shilingi 6,730,515,103**/= sawa na **asilimia 45.** Aidha, Programu hii ilitakiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 1,189,894,000** /= na hadi kufikia Machi 2025 imekusanya jumla ya **Shilingi 1,187,778,908**/= sawa na **asilimia 99.8 (Tafadhali angalia kiambatisho namba 1C na 1D).**

## II. PROGRAMU YA KUSIMAMIA MAENDELEO YA UTALII

41. **Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la programu hii ni kuratibu na kusimamia shughuli za utalii nchini. Matokeo ya muda mrefu ni kuwa na utalii endelevu na wenye tija kwa maslahi ya nchi na wananchi. Huduma zinazotolewa katika

programu hii ni kusimamia utekelezaji wa sera, sheria na mipango ya utalii. Programu hii inatekelezwa na Idara ya Utalii.

## UTEKELEZAJI HALISI

42. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Utalii imeratibu vikao vya pamoja kati ya wajasiriamali wa bidhaa za utalii na wafanyabiashara wa bidhaa za utalii na wenye mahoteli Unguja na Pemba kwa lengo la kutafuta masoko ya uhakika wa bidhaa hizi zinazozalishwa nchini. Kupitia vikao hivyo mafanikio makubwa yameanza kuonekana kwani kwa sasa Wamiliki wa Mahoteli wameanza kununua kutoka kwa wajasiriamali wa kazi za mikono za ususi, ufinyanzi, wakulima wa viungo pamoja na wakulima wa mbogamboga.

43. **Mheshimiwa Spika,** kupitia Kamati za Utalii za Wilaya na Kikosi cha Polisi Utalii na Diplomasia, Idara ya Utalii imeendelea kushiriki katika kupunguza changamoto katika sekta ya utalii nchini, ikiwemo ufanyaji biashara holela katika maeneo ya kitalii, kero ya muziki, pamoja na kutoa elimu na kuwahamasisha wamiliki wa kumbi za starehe kufuata sheria na taratibu zilizowekwa katika kuendesha shughuli za utalii nchini. Kuendelea kufanyika kwa kazi hizi mara kwa mara kunapelekea kutajika vyema kwa nchi yetu ndani na nje ya nchi na kushawishi wageni wengi kuja kutembelea nchini.

44. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Utalii imeratibu kutangazwa kwa utalii wa Zanzibar kwa wajumbe takriban 1000 waliohudhuria mikutano mbalimbali ya Jumuiya za Kitaifa,

Kikanda na Kimataifa kwa mwaka 2024/2025. Miongoni mwa mikutano hiyo ni Mkutano wa Maadhimisho ya Miaka 60 ya Uhusiano wa Kidiplomasia kati ya China na Tanzania, Mkutano wa Kimataifa wa Kupambana na Dawa za Kulevya, Mkutano wa Wahasibu Wakuu wa Serikali wa Afrika na Mkutano wa Mawaziri wa Sheria wa Jumuiya ya Madola. Kupitia mikutano hiyo wajumbe walipata fursa ya kutembelea maeneo mbalimbali ya kihistoria na vivutio vya utalii ili kuweza kujitangaza zaidi.

45. **Mheshimiwa Spika,** katika jitihada za kuimarisha kiwango cha utoaji huduma na ukarimu kwa wageni wanaotembelea nchini, Idara ya Utalii imetoa mafunzo ya watembeza watalii rasmi wapatao 21 katika masuala ya uhifadhi wa bahari, ulinzi na usalama wa watalii na mali zao pamoja na watembeza watalii wasio rasmi 332 kwa lengo la kuwarasimisha. Aidha, Idara kwa kushirikiana na Benki ya NMB imetoa mafunzo kwa wadau 250 wa Unguja na Pemba wanaotoa huduma za utalii wa kiwango cha juu na ujasiriamali wa kutumia mitandao kwa watembeza watalii wapya. Mafunzo haya yanaongeza ujuzi wa kujipatia kipato katika sekta ya utalii.

46. **Mheshimiwa Spika,** ili kuimarisha juhudi za kuifanya Zanzibar kuwa kituo cha utalii wa filamu, Idara imeratibu kurekodiwa kwa filamu ya "Dance Across the World" iliyorekodiwa na Kampuni ya Swahili Safari ya India ambayo ilishirikisha wacheza filamu maarufu wa India akiwemo Mohan Shakti. Filamu hiyo tayari imezinduliwa na kuoneshwa rasmi katika sinema za Bollywood India

ambapo pia imeonekana na mamilioni ya wapenda filamu za kihindi duniani kote. Pamoja na kuvutia watalii kutoka India, filamu hiyo pia imewavutia wacheza filamu na waongoza filamu wengine wa India ya kurekodi filamu zao hapa Zanzibar.

47. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Utalii imeshiriki katika vikao vya kuratibu itifaki za kimataifa zinazohusiana na sekta ya utalii zilizoandaliwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwa moja ya jukumu lake la msingi kwa lengo la kuhakikisha Zanzibar inashirikishwa katika itifaki hizo ambazo zinasimamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hatua hiyo imesaidia Zanzibar kupata fursa ya kushiriki katika mikutano na shughuli mbalimbali zinazohusiana na utalii zinazofanyika kikanda na kimataifa kupitia nafasi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

48. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Utalii imeandaa vipindi vya kuelimisha wananchi kuhusiana na masuala mbalimbali ya kuimarisha utalii, pamoja na kuhamasisha wananchi kushiriki katika shughuli za kitalii na kurusha hewani vipindi mbali mbali vya utangazaji wa utalii katika vituo vya televisheni na mitandao ya kijamii.

49. **Mheshimiwa Spika,** katika kuweka mazingira mazuri ya kazi na wafanyakazi, ili kuleta ufanisi, Idara imepatiwa vitendea kazi vya ofisi ikiwemo kompyuta na printa na vifaa vya kuandikia. Aidha, Idara imelipa stahiki za likizo kwa wafanyakazi tisa na muda wa ziada kwa wafanyakazi wengine.

50. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/2025, programu hii iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 879,000,000**/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2025 imefanikiwa kupata **Shilingi 184,453,619**/= sawa na **asilimia 21.** Jumla ya **Shilingi 273,961654**/= ziliidhinishwa kwa ajili ya mishahara na hadi kufikia Machi 2025 imefanikiwa kupata **Shilingi 198,415,767**/= sawa na **asilimia 72 (tafadhali angalia kiambatanisho namba 1C).**

## III. PROGRAMU YA UTANGAZAJI NA UHAMASISHAJI UTALII

51. **Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la programu hii ni kuongeza uelewa kwa wakaazi wa Tanzania na jamii ya kimataifa kuhusu bidhaa na huduma za utalii zilizopo Zanzibar. Programu hii inatekelezwa na Kamisheni ya Utalii kupitia Idara ya Masoko yenye jukumu la kupanga mikakati na kuitangaza Zanzibar kiutalii ndani na nje ya nchi.

52. **Mheshimiwa Spika**, huduma inayotolewa katika programu hii ni kuitangaza Zanzibar kiutalii ndani na nje ya nchi ili Zanzibar itambulike zaidi kuwa ni kituo bora cha utalii duniani.

## UTEKELEZAJI HALISI

53. **Mheshimiwa Spika,** katika kuitangaza Zanzibar kiutalii ndani na nje ya nchi Kamisheni ya Utalii imeshiriki Maonesho ya Utalii ya Kimataifa ya ITB (Internationale Tourismus Börse) yaliyofanyika mjini Berlin nchini Ujerumani, na Maonesho ya Utalii ya "International

Tourism Market IFTM-TOP RESA" yaliyofanyika mjini Paris nchini Ufaransa. Aidha, katika kuhamasisha utalii wa ndani, Kamisheni ya Utalii imeshiriki katika Maonesho ya Swahili Expo (S!TE) na Maonesho ya Biashara ya Kimataifa (Saba Saba) yaliyofanyika Jijini Dar es Salaam na Maonesho ya Kili Karibu Fair ya Arusha. Kwa upande wa maonesho yanayofanyika Zanzibar, Kamisheni imeshiriki Maonesho ya Kilimo (Nane Nane) ya Kizimbani, Tamasha la Kizimkazi, Maonesho ya Kilimo Hai (Food Organic Festival) huko -Nyamanzi, Kamisheni iliratibu Mashindano ya Kusi Kite Surfing ya Kiwengwa na Tamasha la Vumba lililofanyika Kizingo mjini Unguja. Vile vile, Kamisheni iliandaa Tamasha la Utalii na Utamaduni "Pemba Tourisport Bonanza and Culture" ambalo lilijumuisha michezo na shughuli mbali mbali za utalii ikiwemo mchezo wa ng'ombe, resi za ngalawa, mashindano ya dufu, paredi ya punda, ngoma za asili, ziara katika maeneo ya utalii, kuogelea, resi za kuogelea, kupanda baiskeli na kukimbia (triathlon) na kukimbia na kupanda baiskeli (Duathlon).

54. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua za kuitangaza Zanzibar kimataifa, Kamisheni ya Utalii ilifanikiwa kuandaa maonesho ya Utalii na Uwekezaji (ZTIS) yaliyofanyika Nyamanzi hapa Zanzibar Mwezi wa Oktoba mwaka 2024. Maonesho hayo yalikuwa na lengo la kuwakutanisha wadau na wawekezaji wa sekta ya utalii ili kujadili fursa mbali mbali za utalii zilizokuwa hazijafikiwa na wawekezaji. Aidha, Kamisheni ya Utalii kwa kushirikiana na Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar iliandaa tamasha la "Light Upon Light" na "Halal Tourism" pamoja na kumualika

Mufti Menk kutoka nchini Zimbabwe ambae alifuatana na masheikh Muhammad Salah, Sheikh Wael Ibrahim kutoka Misri, pamoja na Sheikh Ali Hammuda kutoka Uingereza. Tamasha hilo lilikuwa na lengo la kutangaza na kuhamasisha utalii wa maadili hapa Zanzibar.

55. **Mheshimiwa Spika,** Kamisheni ya Utalii kwa kushirikiana na wadau mbali mbali wa utalii imeendelea kuchukua hatua ya kuvitangaza vivutio vya utalii vya Zanzibar ndani na nje ya nchi. Jitihada hizo zimewezesha kuongezeka kwa idadi ya watalii walioingia hapa nchini mwaka 2024 ambapo katika mwaka huo idadi ya watalii walioingia nchini iliongezeka kwa asilimia 15 kutoka watalii 638,498 mwaka 2023 hadi kufikia watalii 736,755 mwaka 2024.

56. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/2025 programu hii iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 972,130,000**/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2025 imefanikiwa kupata **Shilingi 306,899,253**/= sawa na **asilimia 32. (Tafadhali angalia kiambatisho namba 1C).**

## IV. KURATIBU NA KUSIMAMIA MAENDELEO YA UTALII

57. **Mheshimiwa Spika,** lengo la programu hii ni kuongeza tija ya Sekta ya Utalii na kuweka mazingira bora ya rasilimali katika uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa sera na mipango ya utalii. Programu hii imeundwa na programu ndogo mbili ambazo ni:

i. Utawala, Rasilimali Watu na Mipango

ii. Usimamizi na Uratibu wa Shughuli za Utalii

58. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Utawala, Rasilimali Watu na Mipango inatekelezwa na Idara ya Rasilimali Watu, Mipango na Utawala.

**UTEKELEZAJI HALISI**

59. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha upatikanaji wa taarifa za kutosha za watalii wanapoingia nchini Kamisheni ya Utalii kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania, Wizara ya Maliasili na Utalii, Idara ya Uhamiaji na Ofisi ya Taifa ya Takwimu wanaendelea na utafiti wa utokaji wa wageni (Visitors Exit Survey) kwa mwaka 2024. Ripoti hiyo ya utokaji wa wageni kwa sasa ipo katika hatua za uchapishaji na inatarajiwa kutolewa kwa wadau hivi karibuni. Utafiti huo utatoa sura halisi ya ukuaji wa sekta ya utalii hapa nchini, matumizi ya mtalii kwa siku pamoja na siku zao za ukaazi.

60. **Mheshimiwa Spika,** katika kuweka mazingira mazuri ya kazi na wafanyakazi Kamisheni ya Utalii imehakikisha kuwa huduma mbali mbali za uendeshaji wa ofisi zinapatikana pamoja na wafanyakazi kupatiwa stahiki zao. Aidha, safari za kikazi za ndani pamoja na vikao vya mashirikiano na taasisi mbali mbali za Tanzania Bara vimefanyika. Vile vile, Kamisheni ya Utalii imewapatia mafunzo wafanyakazi wake wawili, mmoja anasomea shahada ya pili ya Uongozi wa Biashara (Business Administration)

huko Iringa na mmoja shahada ya kwanza katika Uwekaji wa Kumbukumbu katika Chuo Kikuu cha Zanzibar. Aidha, Kamisheni ya Utalii imeweza kuwapatia wafanyakazi wake 21 mafunzo mbalimbali ya muda mfupi kama vile mafunzo ya udereva, uhasibu, ufuatiliaji na tathmini, utafiti na takwimu, manunuzi, mafunzo ya kutatua migogoro, uhifadhi wa nyaraka na mafunzo ya afya ya akili.

61. **Mheshimiwa Spika,** katika kuendeleza mashirikiano baina ya Kamisheni ya Utalii na Bodi ya Taifa ya Utalii Tanzania (TTB), Kamisheni ya Utalii (ZCT) imeratibu ziara ya Makamishna wa Kamisheni ya Utalii kutembelea maeneo ya vivutio vya utalii vya Ruaha National Park, Isimila na Gans Mkoani Iringa. Ziara hiyo ni miongoni mwa utekelezaji wa mashirikiano yaliyotiwa saini katika MoU baina ZCT na TTB yenye lengo la kubadilishana uzoefu katika masuala ya utalii hapa nchini.

62. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/2025 programu ndogo hii iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 3,104,071,900/=** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2025, imefanikiwa kupata **Shilingi 1,813,828,785/=** sawa na **asilimia 58**, **Shilingi 2,455,878,711/=** kwa ajili ya Mishahara na hadi kufikia Machi 2025 imefanikiwa kupata **Shilingi 1,720,892,686**/= sawa na **asilimia 70** na kutakiwa kukusanya jumla ya **shilingi 12,827,262,611**/= na hadi kufikia Machi 2025, jumla ya **Shilingi 6,610,724,909**/= zimekusanywa sawa na **asilimia 51. (Tafadhali angalia kiambatisho namba 1C na 1D).**

**63. Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Usimamizi na Uratibu wa Shughuli za Utalii inatekelezwa na Idara ya Usimamizi na Uratibu wa Shughuli za Utalii yenye jukumu la kusimamia na kuratibu maendeleo ya utalii nchini.

## UTEKELEZAJI HALISI

**64. Mheshimiwa Spika,** kwa kushirikiana na kikosi cha Polisi Utalii na Diplomasia, maofisa wa Kamisheni ya Utalii wameweza kufanya doria maalumu na za kawaida katika maeneo mbali mbali ya utalii nchini pamoja na kusimamia utoaji huduma za utalii kwa wageni wanaotumia magari ya kubebea utalii. Hadi kufikia mwezi Machi, 2025, Jumla ya doria 620 zimefanyika katika maeneo ya Kizimkazi, Jambiani, Paje, Bwejuu, Michamvi, Unguja Ukuu na Uroa kwa Mkoa wa Kusini Unguja, pamoja na maeneo ya Matemwe, Kiwengwa, Nungwi, Pwani Mchangani na Kendwa kwa Mkoa wa Kaskazini Unguja na maeneo yote ya utalii kwa Mkoa wa Mjini Magharibi.

**65. Mheshimiwa Spika,** katika kutoa huduma zilizo bora za utalii, Kamisheni ya Utalii imewapatia mafunzo watoa huduma za kitalii 300 wakiwemo watembeza watalii, wajasiriamali, na maofisa wa kikosi cha utalii na diplomasia katika maeneo ya Kiwengwa, Matemwe na Nungwi. Mafunzo hayo yana lengo la kuimarisha huduma za utalii kwa kuhakikisha kwamba usalama na mali za wageni wanaowahudumia unaimarika.

**66. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kwamba kampeni ya utalii wa kijani (Greener Zanzibar) inafanikiwa,

Kamisheni ya Utalii imefanya vikao na wadau takriban 150 wa utalii na kutoa elimu juu ya utunzaji wa mazingira ya nchi kavu na baharini, upandaji wa miti pamoja na kusafisha mazingira.

67. **Mheshimiwa Spika,** katika kuwaelimisha wananchi juu ya fursa zinazopatikana katika sekta ya utalii na kuwa na utalii endelevu unaochochea uchumi wa buluu, Kamisheni ya Utalii imeandaa na kurusha vipindi mbali mbali kupitia vyombo vya habari vya Redio na Televisheni. Jumla ya vipindi 53 vimerushwa kupitia redio na televisheni ambavyo ni ZBC redio vipindi 13, ZBC TV vipindi vitano, Bahari FM vipindi viwili, Furaha FM vipindi 12, Clouds FM vipindi vitatu, Mjini FM kipindi kimoja, Crown FM vipindi viwili na Safari Channel vipindi 15.

68. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/2025 programu ndogo hii iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 743,910,000/=** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2025 imefanikiwa kupata **shilingi 250,931,870/=** sawa na **asilimia 34. (Tafadhali angalia kiambatisho namba 1C).**

## V. PROGRAMU YA UENDESHAJI NA MIPANGO KATIKA SEKTA YA UTALII NA MAMBO YA KALE

69. **Mheshimiwa Spika,** programu hii ina jukumu la kusimamia na kuratibu mipango mikuu, sera na tafiti pamoja na usimamizi na uendeshaji mzuri wa rasilimali watu katika Wizara. Programu hii imeundwa na programu ndogo tatu ambazo ni:

i. Utawala na Uendeshaji katika Sekta za Utalii na Mambo ya Kale

ii. Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara

iii. Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba

**70.** **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji katika Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale inatekelezwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi.

**71.** **Mheshimiwa Spika,** huduma zinazotolewa katika programu ndogo ni kujenga uwezo na mazingira mazuri ya kazi kwa wafanyakazi, utayarishaji wa ripoti za fedha na ukaguzi pamoja na mpango wa manunuzi.

## UTEKELEZAJI HALISI

**72.** **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Uendeshaji na Utumishi imefanikiwa kuwajengea uwezo wafanyakazi wake kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi 17 katika fani na ngazi tofauti. **(Tafadhali Angalia Kiambatanisho nambari 2).** Aidha, wafanyakazi 14 wamepata fursa ya kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi. Kadhalika wafanyakazi 210 wamepatiwa mafunzo ya ndani juu ya Utayarishaji na Utekelezaji wa Mkataba wa Huduma kwa Umma, Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma, Mapambano dhidi ya Rushwa na Uhujumu Uchumi na UKIMWI.

**73.** **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Uendeshaji na Utumishi imesimamia ufanyaji wa tathmini ya utendaji kazi wa

wafanyakazi wake wote kwa Unguja na Pemba na kujiridhisha na utendaji wao na kuwaombea nyongeza ya mwaka. Idara pia, imesimamia upandishaji wa madaraja kwa wafanyakazi wanne. Vilevile, Viongozi wa Wizara waliweza kufanya ufuatiliaji utendaji kazi wa shughuli za Wizara kwa upande wa Pemba. Pamoja na kuhudhuria katika vikao kazi vilivyofanyika Dar es Salaam, Dodoma na Arusha. Kadhalika, Idara imeratibu vikao 11 vya Kamati Tendaji na Kamati ya Uongozi ya Wizara kwa ajili ya kujadili Sera, Kanuni, Sheria, Miongozo na Miradi mbali mbali ya maendeleo ya Wizara.

74. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha mashirikiano baina ya Wizara, Taasisi na Mashirika ya Kitaifa na Kimataifa, Wizara imefanya jumla ya vikao 27 na Wadau wa Utalii na Mambo ya Kale wa ndani na nje ya nchi na kujadili maendeleo ya sekta. Kadhalika, katika kuimarisha utekelezaji wa shughuli zake Wizara imeshiriki katika Mkutano wa 24 wa UNESCO ulikofanyika nchini India, Uzinduzi wa Filamu ya Kuitangaza Tanzania "The Amazing Tanzania" katika Soko la China uliofanyika nchini China, Uzinduzi wa Filamu ya kuitangaza Tanzania katika soko la India uliofanyika nchini India na Mkutano wa Nchi za Visiwa uliofanyika nchini Indonesia. Wizara pia, imepokea wageni 22 kutoka mataifa mbali mbali na Mashirika ya Kimataifa kwa lengo la kuimarisha uhusiano mwema na mashirikiano ya utekelezaji wa shughuli za Wizara. Nchi hizo ni Indonesia, Norway, Japan, Italy, Ujerumani, Oman, China, Kenya, Uingereza, Jamaica, pia European Union, na Mashirika ni pamoja na JICA, UNESCO, UNDP, UNICEF,

UNCDF, UNIDO, UNECA, Palladium, World Vegetable Center, Expertise Francais, Global Investor, CNBC Africa, Vattel Academy, National Hospitality Institute of Oman. Wizara ikishirikiana na Jeshi la Polisi Tanzania pamoja na wadau wa maendeleo pia ilifanikiwa kuwasilisha mbele ya Makatibu Wakuu wa SMZ juhudi mbali mbali zinazofanywa na Serikali katika kuimarisha usalama kwa watalii wanaokuja nchini. Kwa mukhtadha huo huo, mnamo tarehe 30 Aprili 2025, Wizara ilipokea msaada wa magari ya usalama wa watalii saba aina ya Quads kutoka Serikali ya Uingereza. Wizara pia hapo awali ilipokea msaada wa pikipiki 10 kutoka Jumuiya ZATI Mwezi wa Septemba mwaka 2024.

75. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/2025, Programu ndogo hii iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 833,200,000**/= kwa kazi za kawaida, hadi kufikia Machi 2025 imefanikiwa kupata **Shilingi 507,452,915**/= sawa na **asilimia 61,** na **Shilingi 953,455,460/=** ziliidhinishwa kwa ajili ya mishahara hadi kufikia Machi 2025 **Shilingi 799,492,838/=** zimepatikana sawa na **asilimia 85. (Tafadhali angalia kiambatisho nambari 1C).**

76. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya kuratibu na kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara inatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti yenye jukumu la kupanga, kutayarisha, kufuatilia na kutathmini Mipango, Sera, Tafiti na Miradi ya Maendeleo ya Wizara.

77. **Mheshimiwa Spika,** huduma ambazo zinatolewa ni uratibu wa sera na tafiti, kuandaa na kuwasilisha Bajeti ya Wizara,

kuandaa na kusimamia mipango na miradi ya maendeleo ya Wizara.

## UTEKELEZAJI HALISI

78. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imeratibu semina maalumu kwa ajili ya Makatibu Wakuu na Manaibu Makatibu Wakuu kwa lengo la kutoa uwelewa mpana juu ya nyaraka mbalimbali zilizowasilishwa wakati wa semina hiyo. Miongoni mwa nyaraka zilizowasilishwa katika semina hizo ni Dhana ya Utalii Endelevu, matokeo ya utafiti wa "Zanzibar Tourism Carring Capacity", Rasimu ya Sheria ya Uanzishwaji wa Mamlaka ya Makumbusho na Urithi wa Mambo ya Kale na Rasimu ya Sera ya Utalii pamoja na Mpango Mkakati wa Utalii wa Zanzibar. Rasimu zote hizo zimejadiliwa kwa kina na kupatiwa maoni na michango ya kutosha na kwa sasa rasimu hizo zinatayarishwa kwa ajili ya kuwasilishwa katika ngazi nyengine ya utekelezaji.

79. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kwamba Dhana ya Utalii Endelevu inafahamika kwa watendaji na maafisa wa Serikali. Idara kwa kushirikiana na taasisi ya "Global Sustainable Tourism Council" imeratibu Mafunzo ya Utalii Endelevu kwa Maafisa Mipango na Maafisa Sera wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na watendaji wa Wizara na taasisi zilizo chini ya Wizara kwa Unguja na Pemba, ili waweze kupanga mipango na sera kwa kuzingatia utalii endelevu pamoja na utunzaji wa mazingira. Kufanya hivyo kutaendeleza kuibakisha nchi katika hali ya ubora

na muonekano wa kuvutia kwa wenyeji na wageni. Aidha, Idara kwa kushirikiana na Taasisi ya Palladium Group chini ya ufadhili wa Serikali ya Uingereza imeandaa muongozo wa kuiwezesha Zanzibar kuwa miongoni mwa vituo bora vya Utalii Endelevu ulimwenguni. Muongozo huo unalenga kuhakikisha kuwa mahoteli na kampuni za waandaaji wa misafara ndani ya Zanzibar wanakidhi viwango vya kimataifa vya utalii endelevu, na hivyo kuchangia Daraja la Mwanzo la asilimia 20 ya utekelezaji wa mpango huo wa kuifanya Zanzibar kuwa kituo bora cha utalii endelevu ndani ya miaka mitatu.

80. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Mipango Sera na Utafiti kwa kushirikiana na Tume ya Uchumi ya Umoja wa Mataifa kwa ajili ya Afrika (UNECA) imeandaa mafunzo ya maafisa wa Serikali juu ya ukusanyaji wa taarifa za mchango wa utalii kwa uchumi wa Zanzibar. Mafunzo hayo yatapelekea kufanyika kwa kazi ya ukusanyaji wa taarifa wa Zanzibar nzima yatakayochambua mchango halisi wa utalii katika uchumi wa nchi.

81. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kwamba utekelezaji wa miradi unafanikiwa kama ilivyopangwa, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imefanya ziara ya kukagua miradi ya maendeleo ambayo ni mradi wa Kuimarisha Eneo la Kihistoria la Mangapwani Unguja na Mradi wa Kuimarisha Eneo la Kihistoria la Ras Mkumbuu Pemba. Utekelezaji wa mradi wa eneo la kihistoria la Mangapwani umefikia **asilimia 90** na utekelezaji wa mradi wa eneo la kihistoria Ras Mkumbuu umefikia **asilimia 60.** Uimarishaji

wa maeneo ya kihistoria una lengo la kuhifadhi, kutunza na kuendeleza historia kwa faida ya vizazi pamoja na kuongeza vivutio vya utalii.

82. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Mipango, Sera, na Utafiti imetayarisha na kuwasilisha Taarifa za Utekelezaji wa Malengo na Shabaha za Mpango wa Maendeleo wa ZADEP katika sekta za Utalii na Mambo ya Kale kwa Tume ya Mipango, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi. Aidha, Idara iliratibu uwasilishaji wa Utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (2020-2025) uliowasilishwa katika Ofisi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) Kisiwandui. Pia, Idara imefanya Ufuatiliaji na Tathmini ya Malengo na Shughuli zinazotekelezwa na Idara na Taasisi za Wizara. Katika ufuatiliaji huo Idara imejiridhisha kwamba taasisi hizo zinatekeleza shughuli zao kwa mujibu wa Mpango Kazi.

83. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/2025, programu ndogo hii iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 250,000,000/=** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2025 imefanikiwa kupata **Shilingi 50,497,953**/= sawa na **asilimia 20,** na iliidhinishiwa **Shilingi 234,242,284** /= kwa ajili ya Mishahara na hadi kufikia Machi 2025 imefanikiwa kupata **Shilingi 160,578,381/**= sawa na **asilimia 69 (Tafadhali angalia kiambatisho namba 1C).**

84. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba inatekelezwa na Ofisi Kuu Pemba.

**85.** **Mheshimiwa Spika,** huduma ambazo zinatolewa ni uratibu wa Sera, Tafiti na Mipango Mikuu ya Ofisi Kuu Pemba, kuratibu Miradi ya Maendeleo na kujenga uwezo na mazingira mazuri ya kazi kwa wafanyakazi.

## UTEKELEZAJI HALISI

**86.** **Mheshimiwa Spika,** katika jitihada za kukifungua Kisiwa cha Pemba Kiutalii, Ofisi Kuu Pemba imeandaa na kufanya Tamasha la Mswahili wa Pemba kwa kushirikiana na wadau wa Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale. Tamasha hilo limefanyika katika viwanja vya Kojani na kumalizikia Wete na kuwajumuisha wenyeji wa maeneo hayo pamoja na wageni kutoka mataifa mbali mbali. Tamasha hilo limeburudishwa kwa ngoma za asili ikiwemo Gonga, Kibati na Msewe pamoja na Michezo ya Asili ikiwemo Resi za Ngarawa na Baskeli. Aidha, Tamasha hilo lilihusisha kuonesha mapishi ya asili yaliyokuwa yakitumika katika miaka tofauti iliyopita. Tamasha hilo la siku mbili lilihudhuriwa na Viongozi mbali mbali wa Serikali, Asasi za Watu Binafsi, Watu mashuhuri pamoja na wananchi wa maeneo ya karibu. Aidha, Ofisi Kuu Pemba imeratibu Maadhimisho ya Siku ya Utalii Duniani yaliyofanyika eneo la Uwanja wa Mpika Tango Mkoani Wilaya ya Mkoani **tarehe 27/09/2024** na yamewashirikisha wananchi kutoka sehemu mbali mbali za Pemba.

**87.** **Mheshimiwa Spika,** Ofisi Kuu Pemba imeratibu ziara za Ufuatiliaji na Tathmini ya utekelezaji wa mradi kupitia programu ya Kuimarisha Maeneo ya Kihistoria kwenye

mradi wa Ras Mkumbuu. Lengo la ziara hizo ni kujadiliana kwa kina uendeshaji na changamoto za utekelezaji wa mradi na hatimae kutatua changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa miradi. Ziara hizo huwashirikisha wahandisi, wataalamu na wasimamizi wa miradi.

88. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi Kuu Pemba imegharamia upatikanaji wa mafunzo ya muda mrefu kwa wafanyakazi watatu katika fani za Uchumi, Utawala na Usimamizi wa Mambo ya Kale na mafunzo ya muda mfupi kwa wafanyakazi watatu katika fani za uhasibu, kumbukubu na udereva. Kupatiwa mafunzo kwa wafanyakazi hao kunasaidia kuimarisha na kukuza utendaji wa kazi pamoja na kuimarisha huduma zinazotolewa kwa wananchi.

89. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua za kuweka mazingira mazuri ya kazi kwa wafanyakazi, Ofisi Kuu Pemba imegharamia upatikanaji wa vifaa vya kuandikia, mafuta, vifaa vya usafi pamoja na kulipia huduma za maji na umeme. Aidha, Ofisi Kuu imelipa stahiki ya likizo kwa wafanyakazi sita pamoja na malipo ya muda wa ziada kwa mfanyakazi mmoja. Vile vile, Ofisi Kuu imewawezesha watendaji kushiriki katika majukumu ya kazi yaliyofanyika kwa upande wa Unguja na Tanzania Bara.

90. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/2025 programu ndogo hii iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 431,400,000**/= kwa ajili ya kazi za kawaida na **Shilingi 562,314,024**/= kwa ajili ya mishahara, hadi kufikia Machi 2025 imefanikiwa kupata **Shilingi 188,816,267**/= kwa kazi

za kawaida sawa na **asilimia 44** na **Shilingi 374,264,601**/= kwa ajili ya mishahara sawa na **asilimia 66.** Programu ndogo hii imetakiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 50,000,000**/=, hadi kufikia Machi 2025, jumla ya **Shilingi 6,497,500**/= zimekusanywa sawa na **asilimia 13. (Tafadhali angalia kiambatisho namba 1C na 1D).**

## J. VIPAUMBELE VYA WIZARA KWA MWAKA 2025/2026.

91. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale pamoja na mambo mengine imepanga kutekeleza vipaumbele vifuatavyo: -

i. Kutekeleza Programu ya Kuimarisha vivutio zaidi vya utalii vilivyopo nchini ili kuweza kuwavutia wageni zaidi.

ii. Kuendelea kukiimarisha Kikosi cha Polisi Utalii ili kiweze kutoa huduma bora.

iii. Kuendelea kuwashawishi wawekezaji kuwekeza katika maeneo ya urithi wa kihistoria na Mambo ya Kale ili yaweze kurudi katika uasili wake na kutunza historia kwa faida ya vizazi vijavyo.

iv. Kuendelea na utekelezaji wa mradi wa Kuimarisha Maeneo ya Kihistoria

v. Kuendelea na mradi wa kuzifanyia matengenezo baadhi ya nyumba zilizopo katika hali mbaya ndani ya eneo la Mji Mkongwe

vi. Kukamilisha mapitio ya Sera ya Utalii pamoja na Mpango Kazi wa Utekelezaji ikiwemo uzinduzi wa Sera ya Makumbusho na Urithi wa Mambo ya Kale

vii. Kukamilisha mapitio ya Sheria ya Utalii ya mwaka 2009 na marekebisho yake ya mwaka 2012.

viii. Kukamilisha mapitio ya Sheria ya Uanzishwaji wa Mamlaka ya Makumbusho na Urithi wa Mambo ya Kale

ix. Kukamilisha utekelezaji wa mapendekezo ya utafiti uliofanywa kitaifa wa Uhimilivu wa Sekta ya utalii Zanzibar (Tourism Carrying Capacity for Zanzibar Study)

x. Ukondoishaji wa viwango vya mfumo wa Utalii Endelevu Duniani (Global Sustainable Tourism Council Standard).

## K. MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

92. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2025/2026, Wizara ya Utalii, na Mambo ya Kale imepangiwa jumla ya **Shilingi 45,032,022,000**/= Kati ya fedha hizo **Shilingi 3,210,300,000**/= ni kwa matumizi ya kawaida, **Shilingi 4,795,900,000**/= kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 37,025,822,000**/= kwa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Aidha, Wizara imepangiwa kukusanya mapato yanayokwenda katika Mfuko Mkuu wa Serikali **Shilingi 2,250,000,000**/=. **(Tafadhali angalia kiambatisho namba 1E, 1F, 1G).**

93. **Mheshimiwa Spika,** katika fedha za mishahara ambazo ni **Shilingi 4,795,900,000**/=, **Shilingi 3,646,500,000**/= kwa ajili ya mishahara ya Wizara na **Shilingi 1,149,400,000**/= ni kwa ajili ya mishahara kwa taasisi za Wizara zinazopokea ruzuku.

94. **Mheshimiwa Spika,** Jumla ya **Shilingi 37,025,822,000**/= zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, kati ya hizo **Shilingi 6,000,000,000/**= zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Kuimarisha Maeneo ya Kihistoria, Shilingi **10,000,000,000** zimetengwa kwa ajili ya mradi wa ukarabati wa nyumba hatarishi zilizomo ndani ya Mji Mkongwe na **Shilingi 6,000,000,000**/= zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza Programu ya kuimarisha vivutio vya Utalii. Aidha **Shilingi 15,025,822,000**/= zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa nyumba ya Beit el Ajaib ambazo ni ufadhili kutoka Serikali ya Ufalme ya Oman. **(Tafadhali angalia kiambatisho namba 1E na 1F).**

95. **Mheshimiwa Spika,** Napenda kuliarifu Baraza lako kuwa, kutokana na kuongezeka kwa vyanzo vya makusanyo vya Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe kumepelekea kuongezeka kwa makusanyo ya Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe. Hivyo, kuanzia mwaka wa fedha 2025/2026 Mamlaka imeruhusiwa kukusanya na kutumia makusanyo yake kwa matumizi mengineyo ambayo ni **Shilingi 3,600,000,000/=**.

96. **Mheshimiwa Spika,** Kamisheni ya Utalii inatarajia kukusanya Shilingi 11,668,715,869/=, kati ya hizo **Shilingi**

**2,000,000,000**/= zitaingizwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina, **Shilingi 2,582,899,269**/= kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 7,085,816,600/**= kwa ajili ya uendeshaji wa kazi za kawaida.

## L. KUWASILISHA BAJETI YA MFUMO WA PROGRAMU (PROGRAM BASED BUDGET - PBB) KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

**97.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale imepangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 45,032,022,000/**= kwa ajili ya kutekeleza programu kuu tano ambazo ni: -

i. Programu ya Maendeleo ya Makumbusho, Mambo ya Kale na Uhifadhi wa Mji Mkongwe. **(Shilingi 34,158,247,000/=)**

ii. Programu ya Kusimamia Maendeleo ya Utalii. **(Shilingi 6,984,182,000/=)**

iii. Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji Utalii. **(Shilingi 1,263,753,800/=).**

iv. Programu ya Uendelezaji na Uratibu wa Utalii. **(Shilingi 10,404,962,096/=).**

v. Programu ya Utawala na Uendeshaji katika Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale. **(Shilingi 3,889,594,000/=).** **(Tafadhali angalia kiambatisho namba 1F)**

**Programu ya Kwanza: Programu ya Maendeleo ya Makumbusho, Mambo ya Kale na Uhifadhi wa Mji Mkongwe**

**98. Mheshimiwa Spika,** programu hii inatekelezwa na Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale pamoja na Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe. Programu hii ina jukumu la kuhakikisha kwamba maeneo ya Kihistoria na Mambo ya Kale yanaendelezwa kwa kuhifadhiwa, kulindwa na kutangazwa pamoja na kuuhifadhi na kuuendeleza Mji Mkongwe ili uendelee kubaki kuwa urithi wa dunia kwa kutoa faida kwa kizazi cha sasa na baadae. Aidha, matokeo ya muda mrefu ya programu hii ni Kuyaimarisha Maeneo ya Kihistoria pamoja na Kuuendeleza Mji Mkongwe. Programu hii imepangiwa jumla ya **Shilingi 34,158,247,000/=.**

**99. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/2026 programu hii inategemea kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kuyahifadhi na kuyaendeleza maeneo ya kihistoria kwa kuyawekea uzio na kuyaimarisha kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na kijamii.

ii. Kuendelea na kuimarisha jitihada za kuwavutia wawekezaji kuwekeza katika maeneo ya kihistoria.

iii. Kuzifanya rasilimali za historia na urithi wa utamaduni kuwa kichocheo cha ukusanyaji wa mapato ya Serikali kupitia shughuli za Utalii.

iv. Uelimishwaji wa jamii katika uhifadhi wa maeneo ya kihistoria na Urithi wa Utamaduni.

v. Kuendelea kutoa ushauri wa kitaalamu na kusimamia Uhifadhi wa Majengo na maeneo ya Mji Mkongwe.

vi. Kuimarisha maeneo, majengo na miundombinu ndani ya Mji Mkongwe.

vii. Kuutangaza Mji Mkongwe kitaifa na kimataifa.

viii. Kuwapatia wafanyakazi mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi.

**100. Mheshimiwa Spika,** ili programu hii iweze kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2025/2026, nawaomba Wajumbe wa Baraza lako kuidhinisha matumizi ya jumla ya **Shilingi 520,370,425/=** kwa kazi za kawaida, **shilingi 2,612,054,575**/= kwa ajili ya mishahara, na **Shilingi 31,025,822,000**/= kwa kazi za Maendeleo. Kati ya fedha hizo **Shilingi 16,000,000,000/=** ni fedha zinazotoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na **Shilingi 15,025,822,000/**= fedha kutoka Serikali ya Ufalme wa Oman. Pia, ninawaomba Wajumbe wa Baraza lako waidhinishe Makusanyo ya Programu hii ya **Shilingi 5,840,000,000/**= kati ya hizo **Shilingi 2,240,000,000/**= zinaingia katika Mfuko Mkuu wa Hazina, **Shilingi 3,600,000,000/**= ni kwa ajili ya matumizi mengineyo kwa Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe.

**Programu ya Pili: Programu ya Kusimamia Maendeleo ya Utalii.**

**101. Mheshimiwa Spika,** programu hii ya Kusimamia Maendeleo ya Utalii inatekelezwa na Idara ya Utalii. Jukumu

la msingi katika programu hii ni Kusimamia na Kuratibu Shughuli za Utalii pamoja na Kuwahamasisha Wananchi juu ya Dhana ya Utalii kwa Wote. Matokeo ya muda mrefu ni kuwa na utalii wenye kuleta manufaa kwa wananchi. Huduma zinazotarajiwa kutolewa ni Uratibu na Uendelezaji wa shughuli za Utalii. Programu hii imepangiwa jumla ya **Shilingi 6,984,182,000/=**

102. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/2026 programu hii inategemea kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kuviendeleza vivutio vipya vya utalii vilivyoibuliwa Unguja na Pemba.

ii. Kuratibu utendaji wa Kamati za Utalii za Wilaya pamoja na wananchi ili kuimarisha utekelezaji wa ehana ya Utalii kwa Wote.

iii. Kuimarisha utolewaji huduma za utalii ili zifikie kiwango cha juu kwa kuelimisha wadau wakiwemo wenye kuandaa misafara ya utalii, watembeza watalii, wajasiriamali wa bidhaa za utalii na waendesha mashamba ya utalii.

iv. Kuimarisha masoko ya bidhaa za kitalii za wajasiriamali wadogo na wa kati kwenye mahoteli na miradi mingine ya kitalii.

v. Kuratibu ushiriki wa Zanzibar katika itifaki za kitaifa na kimataifa zinazohusiana na sekta ya utalii na masuala ya mambo ya kale ikiwemo zinazoratibiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na taasisi nyengine za kitaifa na kimataifa.

vi. Kuratibu mikutano ya wadau yenye lengo la kuzungumzia namna bora ya kuendesha utalii itayoshirikisha wadau wa sekta binafsi na sekta ya umma ili kuondosha kwa ushirikiano changamoto zilizopo na kushirikisha wadau katika mipango ya maendeleo ya sekta ya utalii nchini.

vii. Kuratibu na kushajiisha harakati za maendeleo endelevu ya utalii yenye kuzingatia uhifadhi wa mazingira na kuimarisha usafi katika maeneo ya kitalii Unguja na Pemba.

viii. Kukiimarisha kikosi cha Diplomasia na Utalii ili kiweze kufanya kazi zake kwa ufanisi.

ix. Kuendelea kuwaimarisha wafanyakazi wa Idara ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi ikiwemo mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu, ziara za kimafunzo pamoja na kulipa stahiki za kiutumishi.

**103. Mheshimiwa Spika,** ili programu hii iweze kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2025/2026, ninawaomba Wajumbe wa Baraza lako kuidhinisha matumizi ya jumla ya **Shilingi 694,210,453/=** kwa kazi za kawaida, **Shilingi 6,000,000,000/**= kwa kazi za Maendeleo na **Shilingi 289,971,547/**= kwa ajili ya mishahara.

**Programu ya Tatu: Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji Utalii.**

**104. Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la programu hii ni kuongeza uelewa kwa wakazi wa Tanzania na jamii ya kimataifa

kuhusu bidhaa na huduma za utalii zilizopo Zanzibar. Programu hii inatekelezwa na Kamisheni ya Utalii kupitia Idara ya Masoko yenye jukumu la kupanga mikakati na kuitangaza Zanzibar kiutalii ndani na nje ya nchi.

105. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/2026 programu hii inategemea kutekeleza shughuli zifuatazo : -

i. Kuandaa na kushiriki maonesho, mikutano na makongamano ya utalii ya kitaifa, kikanda na kimataifa ili kuvutia wageni kuvitembelea vivutio vya utalii vya Zanzibar.

ii. Kuwekeza katika utalii wa mikutano (MICE), utalii wa michezo pamoja na utalii wa urithi wa kihistoria.

iii. Kuwaalika waandishi wa habari za utalii wa kimataifa, wamiliki wa mitandao ya kijamii na watu mashuhuri ili Zanzibar ipate fursa ya kutangazwa kupitia watu hawa kwa gharama nafuu.

106. **Mheshimiwa Spika,** ili programu hii iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka wa fedha 2025/2026, nawaomba Wajumbe wa Baraza lako kuidhinisha makusanyo yatakayotumiwa na programu hii ambayo ni jumla ya **Shilingi 1,263,753,800/**= kwa kazi za kawaida.

**Programu ya Nne: Programu ya Uendelezaji na Uratibu wa Utalii.**

107. **Mheshimiwa Spika,** lengo la programu hii ni kuongeza tija ya Sekta ya Utalii na kuweka mazingira bora na rasilimali

watu katika uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa sera na mipango ya utalii. Programu hii inatekelezwa na Kamisheni ya Utalii, ambayo itakuwa na programu ndogo mbili nazo ni: -

i. Utawala, Rasilimali Watu na Mipango

ii. Usimamizi na Uratibu wa Shughuli za Utalii

108. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Utawala, Rasilimali Watu na Mipango, inatekelezwa na Idara ya Rasilimali Watu, Mipango na Utawala. Programu ndogo hii ina lengo la kupanga na kuimarisha uwezo wa Kamisheni ili iweze kutekeleza majukumu yake.

109. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/2026 programu ndogo ya Utawala, Rasilimali Watu na Mipango inategemea kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kufanya utafiti wa utokaji wa wageni ili kufahamu baadhi ya viashiria muhimu vya upimaji wa ukuaji wa sekta ya utalii ikiwemo matumizi ya mtalii kwa siku.

ii. Kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu.

iii. Kuandaa na kuendesha vikao vya Makamishna na Wadau wa Utalii

iv. Kufanya tathmini na kufuatilia shughuli za Kamisheni ya Utalii na Miradi ya Maendeleo.

v. Kufanya mapitio ya Sheria ya Utalii Nambari 6 ya mwaka 2009 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2012 na Kanuni zake.

110. **Mheshimiwa Spika,** ili programu ndogo hii iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka wa fedha 2025/2026, nawaomba Wajumbe wa Baraza lako waidhinishe makusanyo yatakayotumiwa na programu ndogo hii, ambayo ni **Shilingi 2,631,628,800/=** kwa kazi za kawaida, **Shilingi 2,582,899,269**/= kwa ajili ya mishahara. Pia, ninawaomba Wajumbe wa Baraza lako waidhinishe makusanyo ya Programu hii ya **Shilingi 2,000,000,000**/= zitakazoingia Mfuko Mkuu wa Hazina.

111. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Usimamizi na Uratibu na Shughuli za Utalii, inatekelezwa na Idara ya Usimamizi na Uratibu wa Shughuli za Utalii. Programu ndogo hii ina lengo la kusimamia na kuratibu maendeleo ya utalii nchini kwa kushajiisha uwekezaji vitega uchumi katika sekta ya Utalii Zanzibar.

112. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/2026 programu ndogo ya Usimamizi na Uratibu wa Shughuli za Utalii inategemea kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kukagua na kufuatilia miradi ya utalii ili kuhakiki huduma zinazotolewa.

ii. Kuongeza uelewa kwa wananchi kuhusu Sekta ya Utalii pamoja na fursa zinazopatikana kwa kutumia radio, televisheni na makongamano.

iii. Kuandaa mafunzo kwa maofisa watakaofanya kazi ya kuweka viwango vya madaraja kwa bidhaa za utalii kwa vigezo vya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

iv. Kuratibu na kutekeleza Mkakati wa Utalii wa Kijani (Greener Zanzibar) pamoja na Utalii Endelevu.

113. **Mheshimiwa Spika,** ili programu ndogo hii iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka huu wa fedha 2025/2026, ninawaomba Wajumbe wa Baraza lako waidhinishe makusanyo yatakayotumiwa na Programu ndogo hii ya **Shilingi 643,094,000/**= kwa kazi za kawaida.

**Programu ya Tano: Uendeshaji na Mipango katika Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale**

114. **Mheshimiwa Spika,** programu hii ina jukumu la Kusimamia na Kuratibu Mipango Mikuu, Sera na Tafiti pamoja na Usimamizi na Uendeshaji mzuri wa Rasilimali Watu katika Wizara. Matokeo ya muda mrefu ya programu hii ni kuwepo kwa Usimamizi Bora wa Mipango na Uendeshaji wa Rasilimali Watu katika Wizara. Programu hii imepangiwa jumla ya Shilingi 3,889,594,000/= na itasimamia programu ndogo tatu ambazo ni: -

i. Utawala na Uendeshaji katika Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale. **(Shilingi 2,371,576,000 /=)**

ii. Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara. **(Shilingi 478,757,000/=)**

iii. Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji

na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba. **(Shilingi 1,039,261,000/=)**

115. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji katika Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale inatekelezwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi, ambayo ina jukumu la Kusimamia shughuli zote za Utawala, Utumishi, Maendeleo, Wajibu na Maslahi ya Wafanyakazi wa Wizara.

116. **Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la programu ndogo hii ni Usimamizi na Uendeshaji mzuri wa Rasilimali Watu wa Wizara. Huduma zinazotarajiwa kutolewa ni Kujenga uwezo na Mazingira Mazuri ya Kazi kwa Wafanyakazi na Usimamizi wa Mpango wa Manunuzi na Fedha.

117. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/2026 programu ndogo hii inategemea kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kuendelea kuwajengea uwezo wafanyakazi na kuweka mazingira mazuri ya kufanya kazi.

ii. Kupima utendaji kazi wa wafanyakazi wa Wizara kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi wa Wizara.

iii. Kusimamia Utekelezaji wa Mpango wa Manunuzi na kusimamia utekelezaji wa Sheria mpya ya Kanuni ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Umma na Sheria na Kanuni za Fedha.

iv. Kuimarisha Matumizi ya TEHAMA katika utendaji kazi wa Wizara.

v. Kuimarisha mashirikiano baina ya Wadau, Taasisi, Mashirika ya Kitaifa na Kimataifa na Wizara kwa ajili ya Maendeleo ya Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale.

118. **Mheshimiwa Spika,** ili programu ndogo hii iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka wa fedha 2025/2026, ninawaomba Wajumbe wa Baraza lako kuidhinisha matumizi ya jumla ya **Shilingi 1,241,844,598/**= kwa kazi za kawaida na **Shilingi 1,129,731,402/=** kwa ajili ya mishahara.

119. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara inatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti yenye jukumu la Kupanga, Kutayarisha, Kuratibu, Kufuatilia na Kutathmini Mipango, Sera, Tafiti na Miradi ya Maendeleo ya Wizara.

120. **Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la programu ndogo hii ni Kusimamia na Kuratibu Mipango Mikuu, Sera na Tafiti za Wizara. Huduma ambazo zinatarajiwa kutolewa ni Uratibu wa Sera na Tafiti, Kuratibu, Kuandaa Bajeti pamoja na Kuratibu na Kusimamia Mipango na Miradi ya Maendeleo ya Wizara.

121. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/2026 programu ndogo hii inategemea kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kusimamia, Kufuatilia na Kutathimini utekelezaji wa shughuli na Miradi ya Maendeleo ya Wizara.

ii. Kuratibu Vikao vya Ushirikiano kati ya SMZ na SMT kwa Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale.

iii. Kuchapisha na kuzindua Sera za Wizara nazo ni Sera ya Makumbusho na Urithi wa Mambo ya Kale, Sera ya Utalii, Mpango kazi wa Utekelezaji wa Utafiti wa Uhimilivu wa Sekta ya Utalii Zanzibar, Mpango wa Mageuzi wa Urithi wa Mambo ya Kale na Utekelezaji wa Vipaumbele vya Ukondoishaji wa Viwango vya Utalii endelevu vya kimataifa.

iv. Kuendelea kutafuta washirika wa maendeleo watakaoshirikiana na Wizara katika kutekeleza Malengo na Majukumu ya Wizara.

**122. Mheshimiwa Spika,** ili programu ndogo hii iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka huu wa fedha 2025/2026, ninawaomba Wajumbe wa Baraza lako kuidhinisha matumizi ya jumla ya **Shilingi 257,585,260**/= kwa kazi za kawaida na **Shilingi 221,171,740**/= kwa ajili ya mishahara.

**123. Mheshimiwa Spika**, programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba, ina jukumu la Kuhakikisha kuwa Majukumu, Malengo na Shughuli zote za Wizara zilizopangwa zinatekelezwa kwa ufanisi kwa upande wa Pemba.

**124. Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la programu ndogo hii ni Kusimamia na Kuratibu shughuli za Utawala, Uendeshaji na Mipango Mikuu ya Wizara katika Ofisi Kuu-Pemba. Huduma ambazo zinatarajiwa kutolewa ni Uratibu wa Sera,

Tafiti na Mipango Mikuu ya Ofisi Kuu-Pemba, Kuratibu Miradi ya Maendeleo na Kuwajengea Uwezo Wafanyakazi na Mazingira mazuri ya kazi.

125. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/2026 programu ndogo hii inategemea kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kuratibu shughuli zote za Wizara kwa upande wa Pemba.

ii. Kushirikiana na Wadau wa Utalii katika kuifungua na kuitangaza Pemba kwenye sekta ya utalii

iii. Kuhamasisha utalii wa ndani wenye tija kwa wananchi

iv. Kufuatilia na Kutathmini Utekelezaji wa Malengo na Miradi inayotekelezwa Pemba.

v. Kuratibu na kusimamia Matamasha na Matukio ya Utalii na Mambo ya Kale yatakayofanyika Pemba.

vi. Kuwapatia wafanyakazi vitendea kazi vya kutosha ili kuweza kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

126. **Mheshimiwa Spika,** ili programu hii iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka wa fedha 2025/2026, ninawaomba Wajumbe wa Baraza lako kuidhinisha matumizi ya jumla ya **Shilingi 496,290,264/**= kwa kazi za kawaida, **Shilingi 542,970,736/**= kwa ajili ya mishahara. Aidha, ninawaomba Wajumbe wa Baraza lako waidhinishe makusanyo kwa programu ndogo **Shilingi 10,000,000/**= zitakazoingia katika Mfuko Mkuu wa Hazina.

## M. SHUKURANI

127. **Mheshimiwa Spika,** kabla ya kuhitimisha hotuba hii, naomba kutoa shukurani za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuendelea kutupa Ushauri, Miongozo na Maelekezo katika kuziendeleza sekta hizi za Utalii na Mambo ya Kale kwa lengo la kukuza uchumi wa nchi na kuinua kipato kwa wananchi. Aidha, nitumie fursa hii tena kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuteuliwa tena kuwa Mgombea wa Urais wa Zanzibar kupitia Chama Cha Mapinduzi kwa miaka mengine mitano. Nitumie fursa hii kumuomba Mwenye enzi Mungu amjaalie Rais wetu, Afya njema, Hekima, Busara na Uwezo wa kuendelea kutuongoza tena baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2025 na kuendelea kuwatumikia wananchi wa Zanzibar katika kuzidi kuwaletea maendeleo.

128. **Mheshimiwa Spika,** naomba pia kutoa shukurani za kipekee kabisa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuliongoza vyema Taifa la Tanzania chini ya misingi imara ya Muungano wetu, huku akihakikisha kwamba Taifa hili linaendelea kubakia katika hali ya Usalama na Amani, kwa kuzingatia misingi ya Umoja, Upendo na Mshikamano baina yetu. Aidha, naomba nichukue fursa hii kumshukuru tena Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt Samia Suluhu Hassan kwa namna anavyoshiriki kuutangaza utalii

wa nchi kupitia ziara zake za kikazi pamoja na kushiriki katika maonesho na makongamano tofauti yanayofanyika katika mataifa mbali mbali Duniani. Aidha, Nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt, Samia Suluhu Hassan kwa kuteuliwa tena kuwa Mgombea wa Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Chama cha Mapinduzi kwa miaka mengine mitano, huku tukiamini kwamba uteuzi wake untokana na kazi kubwa aliyofanya ya kuleta Mapinduzi ya maendeleo. Tunamuomba Mwenyezi Mungu azidi kumpa Uwezo na Ujasiri wa kulitumikia Taifa hili, huku tukizingatia kauli yake ya ***Kazi Iendelee.***

129. **Mheshimiwa Spika,** shukurani maalumu ziwaendee watendaji Wakuu wa Wizara hii, wakiongozwa na Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Afisa Mdhamini Pemba, Katibu Mtendaji Kamisheni ya Utalii, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe na Wakurugenzi wote kwa kuendelea kunipa ushirikiano wa kutosha katika kutekeleza majukumu yangu ya kila siku. Vile vile, naomba nichukue fursa hii kuwashukuru wafanyakazi wote wa Wizara hii Unguja na Pemba kwa kuendelea kufanya kazi katika misingi ya Uwazi na Uwajibikaji, huku wakihakikisha kwamba Malengo na Majukumu ya Wizara yanafikiwa.

130. **Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee naomba kuwashukuru wadau wote wa Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale Unguja na Pemba kwa jinsi tunavyoendelea kushirikiana nao katika kuhakikisha sekta hizi zinapata maendeleo makubwa na kwa haraka. Aidha, nitumie

hadhira hii, kuwashukuru wamiliki wa vyombo vya habari vya kitaifa na kimataifa pamoja na mitandao ya kijamii, kwa kazi kubwa yenye ubora wa hali ya juu wanayoifanya ya kusaidia kuitangaza Zanzibar na vivutio vya utalii vilivyomo nchini pamoja na kutoa elimu kwa wananchi juu ya uhifadhi na uendelezaji wa Mji Mkongwe na maeneo ya kihistoria. Kufanya hivyo kunachochea kuongezeka kwa idadi ya watalii wanaoingia nchini na kukuza pato la nchi.

131. **Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee ninapenda kuishukuru Ofisi ya Rais Fedha na Mipango pamoja na Tume ya Mipango kwa kuendelea kutupatia miongozo sahihi ya matumizi ya fedha za Serikali kwa manufaa mapana ya wananchi. Aidha, niwashukuru tena kwa kuweza kutupatia fedha kwa ajili ya kufanikisha Malengo na Shughuli za Wizara.

132. **Mheshimiwa Spika,** naomba kuchukua fursa hii ya kipekee kukishukuru Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Wananchi wa Jimbo la Bububu kwa kuendelea kuniamini na kuniunga mkono wakati nikitekeleza majukumu yangu.

133. **Mheshimiwa Spika,** naomba nichukue fursa hii ya kipekee kuishukuru familia yangu yote kwa kuanzia na mke wangu kwa upendo wake, kunisaidia, kunitia moyo na kunivumilia katika utekelezaji wa majukumu yangu. Aidha, nawashukuru wazazi wetu wa pande zote mbili kwa malezi yao yaliyo bora na kutuonesha njia sahihi ya maisha na upendo wao ambao ulituwezesha kufika hapa tulipo. Tunamuomba Mwenye-enzi-Mungu awajaalie maisha

marefu na yenye afya na kuwaombea kwa Mungu aendelee kuzilaza roho za wazazi wetu waliotangulia mbele ya haki malazi mema peponi Amiin.

134. **Mheshimiwa Spika,** naomba uniruhusu nizishukuru Nchi, Mashirika na Taasisi ambazo zimeshirikiana kwa karibu na Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale, pamoja na wadau mbali mbali katika kufanikisha kutekeleza Malengo na Majukumu ya Wizara kupitia sekta zake mbili. Miongoni mwa nchi hizo ni Afrika ya Kusini, Kenya, Oman, Falme za Kiarabu, Qatar, Morocco, Saudi Arabia, China, Japan, Uturuki, Brazil, Uholanzi, Jamhuri ya Korea, India, Uingereza, Marekani, Canada, Italia, Norway, Sweden, Finland, Denmark, Poland, Ureno, Indonesia, Jamaica, Ujerumani na Ufaransa.

135. **Mheshimiwa Spika,** naomba niishukuru Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afirika Mashariki kwa kuendelea kuitangaza Tanzania ikiwemo Zanzibar katika safu za Utalii za Kimataifa. Kipekee niwashukuru sana Mabalozi wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania waliopo katika mataifa mbali mbali na wanaoendelea kuitangaza Zanzibar kupitia Diplomasia ya Uchumi.

136. **Mheshimiwa Spika,** naomba nichukuwe fursa hii kuwashukuru Mashirika, Taasisi na Jumuiya za Kimataifa zikiwemo World Bank, JICA, UNESCO, UNDP, UNICEF, UNCDF, UNIDO, UNECA, GSTC, EU, TBI, USAID, Palladium, World Vegetable Centre na Expertise Francais. Pia Jarida la Global Investor na Kituo cha CNBC Africa.

Ambavyo vimetoa mchango mkubwa wa kuwasilisha ujumbe wa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuhusiana na Sekta ya Utalii Zanzibar kwa mahujiano ya moja kwa moja nae na kuwafikia wasomaji na watazamaji wengi Ulimwenguni. Aidha, nizishukuru Taasisi za ndani zikiwemo ZATI, ZATO, ZATOGA, HAZ, NMB, PBZ, PDB TANAPA, Kituo cha Zanzibar Cable TV, pamoja na ZBC na vituo vyengine vya habari ndani na nje ya nchi kwa mchango wao mkubwa katika kuitangaza Sekta ya Utalii. Halikadhalika, Jumuiya ya Kanisa la Anglikana, Jumuiya ya "Light upon Light" ya Mufti Menki, Mwambao Coastal Community Network Tanzania, Chumbe Island Coral Park (CHICOP) na Infinity Develelopment LTD.

137. **Mheshimiwa Spika,** mwisho naomba kukushukuru wewe binafsi, pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako kwa kunisikiliza kwa Utulivu, Umakini na Usikivu wa hali ya juu.

## N. MAOMBI YA FEDHA KWA AJILI YA KUTEKELEZA PROGRAMU ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

138. **Mheshimiwa Spika,** ninawaomba Wajumbe wa Baraza lako kujadili kwa kina matumizi ya jumla ya Wizara ya **Shilingi 45,032,022,000/**=. Kati ya hizo **Shilingi 3,210,300,000/**= kwa kazi za kawaida, **Shilingi 4,795,900,000**/= kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 37,025,822,000**/= kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Aidha, naomba Wajumbe wa Kamati yako waidhinishe makusanyo ya

mapato ya **Shilingi 2,250,000,000/**= kwa fedha zinazoingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

139. **Mheshimiwa Spika,** ninawaomba Wajumbe wa Baraza lako kuidhinisha makusanyo ya **Shilingi 11,668,715,869/**= ambazo zitakusanywa na Kamisheni ya Utalii, kati ya hizo **Shilingi 2,000,000,000/**= zitaingizwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina, **Shilingi 2,589,899,269/**= kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 7,085,816,600**/= kwa ajili ya uendeshaji wa kazi za kawaida.

140. **Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe imeruhusiwa kukusanya na kutumia fedha zinazotokana na vyanzo vyake vya mapato, nawaomba Wajumbe wa Baraza lako waidhinishe makusanyo ya **Shilingi 3,600,000,000/**= kwa ajili ya shughuli mbali mbali za utekelezaji na utoaji huduma kupitia Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe.

## O. HITIMISHO

**141. Mheshimiwa Spika,** kwa heshima na taadhima nawaomba Wajumbe wa Baraza lako Waipokee, Waijadili, Watushauri, Watuelekeze na baadae Waipitishe bajeti hii ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale.

**142. Mheshimiwa Spika,** Naomba Kutoa Hoja.



# VIAMBATISHO

Kiambatisho Namba 1A

## MAPATO YALIOKUSANYWA JULAI 2024 HADI MACHI 2025
## MAPATO YANAYOINGIA HAZINA

| TAASISI | BAJETI 2024/2025 | MAPATO YALIOKUSANYWA JULAI 2024 HADI MACHI 2025 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale | 900,000,000.00 | 1,187,778,908.00 | **131.98** |
| Ofisi Kuu Pemba | 50,000,000.00 | 6,507,500.00 | **13.02** |
| Mamlaka ya Mji Mkongwe | 289,894,000.00 | - | **-** |
| **JUMLA NDOGO** | **1,239,894,000.00** | **1,194,286,408.00** | **96.32** |
| Kamisheni ya Utalii | 12,827,262,611 | 6,610,724,909 | 51.00 |
| **JUMLA NDOGO** | **12,827,262,611** | **6,610,724,909** | **51.00** |
| **JUMLA KUU YA WIZARA** | **14,067,156,611.00** | **7,805,011,317.00** | **55.48** |

KIAMBATISHO NAMBA 1B

TAASISI ZISIZOPOKEA RUZUKU

| TASISI | MAELEZO | BAJETI YA JULAI 2024- 2025 | FEDHA ZILIZOPATIKANA JULAI - MACHI 2024/2025 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| Ofisi kuu Pemba | Mishahara | 562,314,030.00 | 374,264,601.00 | **67%** |
| | M/Mengineyo | 431,400,000.00 | 145,816,267.00 | **34%** |
| **JUMLA** | | **993,714,030.00** | **520,080,868.00** | **52%** |
| Idara ya Mipango, Sera na Utafiti | Mishahara | 234,242,384.00 | 160,578,381.00 | **69%** |
| | M/Mengineyo | 250,000,000.00 | 50,497,953.38 | **20%** |
| **JUMLA** | | **484,242,384.00** | **211,076,334.38** | **44%** |
| Idara ya Uendeshaji na Utumishi | Mishahara | 943,455,460.00 | 799,492,838.00 | **85%** |
| | M/Mengineyo | 833,200,000.00 | 507,452,915.39 | **61%** |
| **JUMLA** | | **1,776,655,460.00** | **1,306,945,753.39** | **74%** |
| Idara ya Utalii | Mishahara | 273,961,654.00 | 198,415,767.00 | **72%** |
| | M/Mengineyo | 879,000,000.00 | 184,453,619.84 | **21%** |
| **JUMLA** | | **1,152,961,654.00** | **382,869,386.84** | **33%** |
| Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale | Mishahara | 1,486,226,472.00 | 1,030,330,225.50 | **69%** |
| | M/Mengineyo | 649,600,000.00 | 122,187,728.55 | **19%** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **JUMLA** | | **2,135,826,472.00** | **1,152,517,954.05** | **54%** |
| **JUMLA MISHAHARA** | | **3,500,200,000.00** | **2,563,081,812.50** | **73%** |
| **JUMLA MATUMIZI MENGINEO** | | **3,043,200,000.00** | **1,010,408,484.16** | **33%** |
| **JUMLA KU KWA TAASISI ZISIZOPOKEA RUZUKU** | | **6,543,400,000.00** | **3,573,490,296.66** | **55%** |

**TAASISI ZA RUZUKU**

| **TAASISI** | **MAELEZO** | **BAJETI YA JULAI-JUNI 2024 - 2025** | **FEDHA ZILIZOPATIKANA JULAI - MACHI 2024/2025** | **ASILIMIA** |
|---|---|---|---|---|
| Mamlaka ya Mji Mkongwe | Mishahara | 1,088,170,000.00 | 828,714,621.00 | **76%** |
| | M/Mengineyo | 375,600,000.00 | 97,610,407.00 | **26%** |
| | | 1,463,770,000.00 | 926,325,028.00 | **63%** |
| **JUMLA YA MISHAHARA YA RUZUKU** | | **1,088,170,000.00** | **828,714,621.00** | **76%** |
| **JUMLA YA MATUMIZI MENGINEO** | | **375,600,000.00** | **97,610,407.00** | **26%** |
| **JUMLA KUU YA RUZUKU** | | **1,463,770,000.00** | **926,325,028.00** | **63%** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **JUMLA YA MISHAHARA KWA WIZARA** | | **4,588,370,000.00** | **3,391,796,433.50** | **74%** |
| **JUMLA YA MATUMIZI MENGINEYO KWA WIZARA** | | **3,418,800,000.00** | **1,108,018,891.16** | **32%** |
| **JUMLA KUU YA WIZARA (MATUMIZI YA KAWAIDA)** | | **8,007,170,000.00** | **4,499,815,324.66** | **56%** |
| **MIRADI YA MAENDELEO** | | | | |
| Kuimarisha maeneo ya kihistoria | | **39,025,822,000.00** | **852,468,702.00** | **2%** |
| **JUMLA KUU YA WIZARA (MIRADI YA MAENDELEO)** | | **39,025,822,000.00** | **852,468,702.00** | **2%** |
| **JUMLA KUU YA WIZARA** | | **47,032,992,000.00** | **5,352,284,026.66** | **11%** |

**KAMISHENI YA UTALII**

| TAASISI | MAELEZO | BAJETI YA JULAI-JUNI 2024 - 2025 | FEDHA ZILIZOPATIKANA JULAI - MACHI 2024/2025 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| Kamisheni ya Utalii | Mishahara | 2,455,878,711.00 | 1,720,892,686.00 | **70%** |
| | M/Mengineyo | 4,820,111,900.00 | 2,371,659,908.00 | **49%** |
| **JUMLA NDOGO** | | **7,275,990,611.00** | **4,092,552,594.00** | **56%** |
| **JUMLA YA MISHAHARA** | | **2,455,878,711.00** | **1,720,892,686.00** | **70%** |
| **JUMLA YA MATUMIZI MENGINEO** | | **4,820,111,900.00** | **2,371,659,908.00** | **49%** |
| **JUMLA KUU YA KAMISHENI YA UTALII** | | **7,275,990,611.00** | **4,092,552,594.00** | **56%** |

## FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2024 HADI MACHI 2025 KWA KILA PROGRAMU NDOGO

**Programu ndogo ya Uendelezaji wa Urithi wa Mambo ya Kale**

| TAASISI | BAJETI 2024/2025 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2024 HADI MACHI 2025 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| **Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale** | 41,161,648,472.00 | 2,004,986,656.05 | **4.87** |
| **Mamlaka ya Mji Mkongwe** | 1,463,770,000.00 | 926,325,028.00 | **63.28** |
| **JUMLA** | **42,625,418,472.00** | **2,931,311,684.05** | **6.88** |

**Programu ndogo ya Kuratibu na Kuendeleza Utalii**

| TAASISI | BAJETI 2024/2025 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2024 HADI MACHI 2025 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| **Idara ya Utalii** | 1,152,961,654.00 | 382,869,386.84 | **33.21** |
| **JUMLA** | **1,152,961,654.00** | **382,869,386.84** | **33.21** |

**Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji Utalii**

| TAASISI | BAJETI 2024/2025 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2024 HADI MACHI2025 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| **Kamisheni ya Utalii (Idara ya Masoko)** | 972,130,000,00 | 306,899,253.00 | **31.5** |
| **JUMLA** | **972,130,000,00** | **306,899,253.00** | **31.5** |

**Programu ya Kuratibu na Kusimamia Maendeleo ya Utalii**

| TAASISI | BAJETI 2024/2025 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2024 HADI MACHI 2025 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Kamisheni ya Utalii (Idara ya Mipango) | 6,303,860,611.00 | 3,785,653,341.00 | **60.00** |
| **JUMLA** | **6,303,860,611.00** | **3,785,653,341.00** | **60.00** |

**Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji Katika Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale**

| TAASISI | BAJETI 2024/2025 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2024 HADI MACHI2025 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Idara ya Uendeshaji na Utumishi | 1,776,655,460.00 | 1,306,945,753.39 | **73.56** |
| **JUMLA** | **1,776,655,460.00** | **1,306,945,753.39** | **73.56** |

**Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamisha Mipango Mikuu ya Wizara**

| TAASISI | BAJETI 2024/2025 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2024 HADI MACHI 2025 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Idara ya Mipango Sera na Utafiti | 484,242,384.00 | 211,076,334.38 | **43.59** |
| **JUMLA** | **484,242,384.00** | **211,076,334.38** | **43.59** |

**Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba**

| TAASISI | BAJETI 2024/2025 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2024 HADI MACHI 2025 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Ofisi Kuu Pemba | 993,714,030.00 | 520,080,868.00 | **52.34** |
| **JUMLA** | **993,714,030.00** | **520,080,868.00** | **52.34** |

*Kiambatisho Namba 1D*

**FEDHA ZILIZOKUSANYWA JULAI 2024 HADI MACHI 2025 KWA KILA PROGRAMU NDOGO**

**Programu ndogo ya Uendelezaji wa Urithi wa Mambo ya Kale**

| TAASISI | BAJETI 2024/2025 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2024 HADI MACHI 2025 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale | 900,000,000.00 | 1,187,778,908.00 | **131.98** |
| Mamlaka ya Mji Mkongwe | 289,894,000.00 | - | - |
| **JUMLA** | **1,189,894,000.00** | **1,187,778,908.00** | **99.82** |

**Programu ya Kuratibu na Kusimamia Maendeleo ya Utalii**

| TAASISI | BAJETI 2024/2025 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2024 HADI MACHI 2025 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Kamisheni ya Utalii (Idara ya Mipango) | 12,827,262,611 | 6,610,724,909 | **51.00** |
| **JUMLA** | **12,827,262,611** | **6,610,724,909** | **51.00** |

**Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba**

| TAASISI | BAJETI 2023/2024 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2023 HADI MACHI 2024 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Ofisi Kuu Pemba | 50,000,000.00 | 6,507,500.00 | **13.02** |
| **JUMLA** | **50,000,000.00** | **6,507,500.00** | **13.02** |

*Kiambaticho Namba 1E*

**BAJETI INAYOOMBWA NA WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026**

| MAELEZO | MAELEZO | BAJETI YA JULAI-JUNE 2025- 2026 |
|---|---|---|
| Ofisi kuu Pemba | Mishahara | 542,970,736.00 |
| | M/Mengineyo | 496,290,264.00 |
| **JUMLA** | | **1,039,261,000.00** |
| | Mishahara | 221,171,740.00 |
| Idara ya Mipango, Sera na Utafiti | M/Mengineyo | 257,585,260.00 |
| **JUMLA** | | **478,757,740.00** |
| | Mishahara | 1,129,731,402.00 |
| Idara ya Uendeshaji na Utumishi | M/Mengineyo | 1,241,844,598.00 |
| **JUMLA** | | **2,371,576,000.00** |
| | Mishahara | 289,971,547.00 |
| Idara ya Utalii | M/Mengineyo | 694,210,453.00 |
| **JUMLA** | | **984,182,000.00** |
| | Mishahara | 1,462,654,575.00 |
| Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale | M/Mengineyo | 520,370,425.00 |
| **JUMLA** | | |

| | | |
|---|---|---|
| | | **1,983,025,000.00** |
| **JUMLA MISHAHARA** | | **3,646,500,000.00** |
| **JUMLA MATUMIZI MENGINEO** | | **3,210,300,000.00** |
| **JUMLA KU KWA TAASISI ZISIZOPOKEA RUZUKU** | | **6,856,800,000.00** |

**TAASISI ZA RUZUKU**

| MAELEZO | MAELEZO | BAJETI YA JULAI-JUNE 2025- 2026 |
|---|---|---|
| Mamlaka ya Mji Mkongwe | Mishahara | 1,149,400,000.00 |
| | M/Mengineyo | - |
| | | |
| **JUMLA YA MISHAHARA YA RUZUKU** | | **1,149,400,000.00** |
| **JUMLA YA MATUMIZI MENGINEO** | | **-** |
| **JUMLA KUU YA RUZUKU** | | **1,149,400,000.00** |
| **JUMLA YA MISHAHARA KWA WIZARA** | | **4,795,900,000.00** |
| **JUMLA YA MATUMIZI MENGINEYO KWA WIZARA** | | **3,210,300,000.00** |
| **JUMLA KUU YA WIZARA (MATUMIZI YA KAWAIDA)** | | **8,006,200,000.00** |
| **MIRADI YA MAENDELEO** | | |
| Programu ya Kuimarisha maeneo ya kihistoria | | **6,000,000,000.00** |
| Ukarabati wa nyumba za Mji | | **10,000,000,000.00** |

| | | |
|---|---|---|
| Mkongwe | | |
| Programu ya kuimarisha vivutio vya Utalii | | **6,000,000,000.00** |
| Ukarabati wa Beit Al Ajaib | | **15,025,822,000.00** |
| **JUMLA KUU YA WIZARA (MIRADI YA MAENDELEO)** | | **37,025,822,000.00** |
| **JUMLA KUU YA WIZARA** | | **45,032,022,000.00** |

**KAMISHENI YA UTALII**

| MAELEZO | MAELEZO | BAJETI YA JULAI-JUNI 2025- 2026 |
|---|---|---|
| **Kamisheni ya Utalii** | **Mishahara** | 2,582,899,269.00 |
| | **M/mengineyo** | 7,085,816,600.00 |
| **JUMLA** | | **9,668,715,869.00** |
| **JUMLA YA MSHAHARA** | | **2,582,899,269.00** |
| **JUMLA YA MATUMIZI MENGINEYO** | | **7,085,816,600.00** |
| **JUMLA KUU YA KAMISHENI YA UTALII** | | **9,668,715,869.00** |

*Kiambatisho Namba 1F*

## BAJETI INAYOOMBWA NA WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

**Programu ndogo ya Uendelezaji wa Urithi wa Mambo ya Kale**

| TAASISI | BAJETI 2025/2026 MATUMIZI | BAJETI 2025/2026 MAPATO |
|---|---|---|
| **Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale** | 7,983,025,000.00 | 4,533,539,000.00 |
| **Mamlaka ya Mji Mkongwe** | 26,175,222,000.00 | - |
| **JUMLA** | **34,158,247,000.00** | **4,533,539,000.00** |

**Programu ndogo ya Kuratibu na Kuendeleza Utalii**

| TAASISI | BAJETI 2025/2026 MATUMIZI | BAJETI 2025/2026 MAPATO |
|---|---|---|
| Idara ya Utalii | 6,984,182,000.00 | - |
| **JUMLA** | **6,984,182,000.00** | **-** |

**Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji Utalii**

| TAASISI | BAJETI 2025/2026 MATUMIZI | BAJETI 2025/2026 MAPATO |
|---|---|---|
| Kamisheni ya Utalii (Idara ya Masoko) | 1,263,753,800.00 | - |
| **JUMLA** | **1,263,753,800.00** | **-** |

-

**Programu ya Kuratibu na Kusimamia Utalii**

| TAASISI | BAJETI 2025/2026 MATUMIZI | BAJETI 2025/2026 MAPATO |
|---|---|---|
| Kamisheni ya Utalii (Idara ya Mipango) | 6,404,962,069.00 | 11,668,715,869.00 |
| **JUMLA** | **6,404,962,069.00** | **11,668,715,869.00** |

**Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji Katika Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale**

| TAASISI | BAJETI 2025/2026 MATUMIZI | BAJETI 2025/2026 MAPATO |
|---|---|---|
| Idara ya Uendeshaji na Utumishi | 2,371,576,000.00 | |
| **JUMLA** | **2,371,576,000.00** | **-** |

**Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamisha Mipango Mikuu ya Wizara**

| TAASISI | BAJETI 2025/2026 MATUMIZI | BAJETI 2025/2026 MAPATO |
|---|---|---|
| Idara ya Mipango Sera na Utafiti | 478,757,000.00 | - |
| **JUMLA** | **478,757,000.00** | **-** |

**Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba**

| TAASISI | BAJETI 2025/2026 MATUMIZI | BAJETI 2025/2026 MAPATO |
|---|---|---|
| Ofisi Kuu Pemba | 1,039,261,000.00 | 50,000,000.00 |
| **JUMLA** | | |
| | **1,039,261,000.00** | **50,000,000.00** |

## MAKADIRIO YAMAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

## MAPATO YANAYOINGIA HAZINA

| TAASISI | BAJETI 2025/2026 |
|---|---|
| Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale | 2,250,000,000.00 |
| Ofisi Kuu Pemba | 10,000,000.00 |
| **JUMLA NDOGO** | **2,250,000,000.00** |
| Kamisheni ya Utalii | 2,000,000,000.00 |
| **JUMLA NDOGO** | 2,000,000,000.00 |
| **JUMLA** | **4,250,000,000.00** |

**KIAMBATISHO 2**

| ORODHA YA WATUMISHI WA WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE WALIOFATA FURSA YA MASOMO KWA MWAKA 2024/2025 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **S/N** | **JINA KAMILI** | **JINSIA** | **CHUO** | **FANI ANAYOSOMEA** |
| 1 | Nd. Hawa Sheha Haji | Mke | Harbin University of Commercial - China | Shahada ya Pili ya Uongozi wa Utalii na Hotel |
| 2 | Nd. Rukaiya Ali Abdulrahman | Mke | Harbin Institute of Technology - China | Shahada ya Pili ya Uongozi wa Kibiashara |
| 3 | Nd. Khamis Salim Khamis | Mme | Yunnan University - China | Shahada ya Pili ya Project Management |
| 4 | Nd. Khamis Sheha Haji | Mme | Dibrugarh Universirty - India | Phd ya Anthropology |
| 5 | Nd. Mgeni Juma Khamis | Mke | Eskisehir Osmangazi University - Uturuki | Phd ya Utalii |
| 6 | Nd. Sharifa Rashid Nderema | Mke | Beijing jiaotong University - China | Shahada ya Pili ya Urban and Rural Planning |
| 7 | Nd. Laila Bakar Mohammed | Mke | ICPS | Cheti cha Business Operation Assistance |
| 8 | Nd. Saleh Omar Abdalla | Mme | Karume | Cheti cha Plumbing and pipe Fitting |
| 9 | Nd. Omar Moh'd Bakar | Mme | Karume | Cheti cha Plumbing and pipe Fitting |
| 10 | Nd. Ujuddi Mustafa Khamis | Mme | Zanzibar University | Shahada ya Pili ya Supplies and Procurement Management |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 11 | Nd. Ali Hamad Ali | Mme | Ardhi University | Shahada ya Pili ya Urban Planning and Management |
| 12 | Nd. Hamad Rajab Hamad | Mme | State University of Zanzibar (SUZA) | Shahada ya Pili ya Heritage Management and Marketing |
| 13 | Nd. Fatma Asaa Sharif | M'ke | Mount Kenya | Shahada ya Kwanza ya Rasilimali Watu |
| 14 | Nd. Abdalla Omar Khalifa | M'me | Yunnan University- China | Shahada ya Pili ya Economics |
| 15 | Nd. Ame Mrisho Hilal | Mme | Micro Teaching | Cheti cha ICT |
| 16 | Nd. Ali Haidar Hashim | Mme | Mysori University India | Shahada ya Pili ya Uwekezaji na Uongozi |
| 17 | Nd. Asha Juma Nyendo | Mke | Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere | Stashahada ya Uchumi (Economics) |